# MASWALI YA KISWAHILI FASIHI

For Answers, prefer calling Mdm Mariam-0746711892

Setbooks summarised notes,questions and vedios are available.Contact Mdm.Mariam-0746711892






© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

# 102/3 - KISWAHILI - Paper 3

## Karatasi ya Tatu

## SEHEMU YA KWANZA

MTIHANI 1

SEHEMU YA A:TAMTHILIA

Majoka alitumia njia nyingi kudhibiti uongozi wake. Thibitisha ukweli huu. (alama 20

SEHEMU B: RIWAYA

1. Wanawake wamesawiriwa kwa mtazamo chanya katika jamii ya chozi la Heri. Jadili ukweli huu kwa kutoa ithibati mwafaka. (alama. 20)
2. "Ni mara ngapi mimi na babako husafiri na kukupagaza ulezi wa ndugu zako hawa? …umeweza kumuelekeza… katika kipindi hiki ambacho anatafuta utambuaji. Wewe pekee ndiwe dawa ya hasira … ya kivolkano. Bila wewe malezi ya hawa wadogo wako yangekuwa magumu.

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b)Tambulisha mbinu tatu za sanaa zilizotumika katika dondoo hili. (alama 3)

c)Eleza sifa sita za mhusika "babako" aliyerejelewa katika dondoo hili. (alama 6)

d) "Ulezi ni ujima". Thibitisha kauli hii kwa kurejelea dondoo hili na riwaya yote kwa jumla. (alama 7)

SEHEMU YA C:HADITHI FUPI *Kochokocho A na D. Kayanda(Wah.): (Tumbo Lisilishiba na Hadithi Nyingine)*

3. Jadili matatizo yanayokumba sekta ya elimu huku ukirejelea hadithi zozote tano katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba. (alama. 20)
4. "…hata mapenzi yako yawe mazito namna gani…ni bora kuliko kasoro ya mapenzi."

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

b)Tathmini umuhimu wa mnenewa. (al 6)

c)Thibitisha ukweli kuwa mapenzi yanayorejelewa yaligeuka na kuwa mazito kuliko ilivyotarajiwa na yakawa na kasoro nyingi. (al.10

SEHEMU YA D: USHAIRI



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724251706)

*Jibu swali la 6 au 7*

5. *Soma shairi hili kisha ujibu maswali.* Jicho, tavumiliaje, kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo
Kwacho, lijalo na lije, nimechoka vumiliyo
Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhui tuyasikiayo
Nayo, visa na mauko, wanyonge
wayakutayo Kwayo, sina zuiliko, natoa
niyahisiyo Naandika!

Hawa, wanotulimiya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaoumiya, na maafa wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine,kwao liko angamiyo
Hawa, uwapa unene, watukufu wenye nayo
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tafauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado , tuling'owe shina, ulaji pia na moyo
Naandika!

Maswali

a) Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari zipi? Thibitisha kila jibu lako (ala4)
b) Eleza dhamira ya mshairi (ala2)
c) Onyesha mifano miwili ya uhuru wa kishairi jinsi ulivyotumika katika shairi (ala2)
d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (al.4)
e) Tambulisha kwa mifano mbinu zozote mbili za sanaa katika shairi. (ala2)
f) Fafanua sifa za kiarudhi zilizotumika katika ubeti wa tano. (al.3)
g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. (ala3) i) Zuiliko ii) Wavune iii) Wenye pupa na kamiyo.

6. *Soma shairi hili kisha ujibu maswali.*
Amka!
Uondoe utandu machoni
Uone mtandao duniani
Uchawi wa karne hii
Uunganishavyo watu.



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Amka!
Uwe mtu mpya
Uabiri mtandao ulimwenguni
Ukuvushe milima na mabonde
Ujuane na watu.

Amka!
Uwe na yako anwani
Udhibiti wavuti mkononi
Uone na uonekane kote
Uzungumze na watu
Ufurahie malimwengu

Amka!
Uone huu ulimwengu
Ulivyofanywa mdogo sasa
Ulivyopea kimawasiliano
Unganike na watu.

Amka!
Ukalie tarakilishi
Uangaze usioyajua
Uwasiliane kwa meme
Uunganike na watu.

Amka!
Uone nukulishi
Ubebe yako rununu
Useme na ulimwengu
Useme na watu

<u>Maswali</u>

a)Lipe shairi hili anwani mwafaka. (al. 2 b)Shairi hili ni la aina gani? Thibitisha. (al.2 c)Andika maneno manne yanayotaja teknolojia ya kisasa. (al.2 d)Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari. (al.4

e)Eleza toni ya shairi hili. (al.2

f)Tambulisha nafsi neni na nafsi nenewa. (al.2

g)Tambulisha kwa mifano mbinu mbili za lugha katika shairi hili. (al.2

h)Ni nini maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumika katika shairi. (al.4 ) i) Uchawi wa karne katika shairi



© 2019 BWANA CHEBKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

ii) Ukavushe milima na mabonde

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

(a) Eleza sifa nne za kimtindo zinazopatikana katika methali za Kiswahili. (alama 8)

(b) Eleza mbinu tatu ambazo hutumiwa kuzua misimu. (alama 6)

(c) Ni jukumu la jamii kudumisha fasihi simulizi. Dhihirisha. (alama 6)

MTIHANI 1

RIWAYA: CHOZI LA HERI (Assumpta K. Matei)

1. "… wino wa Mungu haufutiki…"
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)
   (b) Taja na uelembinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hii (alama 2)
   (c) Fafanua ukweli wa kauli hii kwa kuzingatia hoja zozote kumi na nne kutoka katika riwaya ya Chozi la Heri (alama 14)

TAMTHILIA: KIGOGO(Pauline Kea)

2. "Mambo yamekwenda kombo Sagamoyo, sio siri tena."
   (a) Fafanua sifa na umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya (alama 6)
   (b) Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja kumi nan ne kutoka katika tamthilia ya kigogo (alama 14)
3. "Ushahidi itatoka wapi kama kipanga ndiye hakimu kwenye kesi ya kuku?"
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)
   (b) Fafanua mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hii (alama 4)
   (c) Fafanua haki kumi na mbili za Wanasagamoyo na uonyeshe jinsi ziivyokiukwa (alama 12)

HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

4. "… Basi niache nitafute pesa. Muhimu mniunge mkono…"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   (b) Fafanua sifa zozote nne za mzungumziwa (alama 4)
   (c) Fafanua athari ya vitendo vya mzungumzaji wa maneno haya katika jamii (alama 12)
5. Jadili suala la uozo wa maadili katika jamii huku ukirejelea hadithi zozote nne katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine (alama 20)

USHAIRI

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu masuali*

Ujuaji kwa fasili, kujifanya watambua,
Ujuaji kiwasili, majitapa huwadia,
Ujuaji kwa asili, kujibeba bila nia,
Ujuaji jambo kali, binadamu



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

tagundua.

Ujuaji kila hali, usijitie wajua,
Ujuaji takudhuli, matatani kutumbua,
Ujuaji si mwimili, wa Mungu kudurua,
Ujuaji jambo kali, binadamu tagundua.

Ujuaji mkatili, elimuni kubagua,
Ujuaji tafisili, zako mali kupungua,
Ujuaji kiakili, epukana julangua,
Ujuaji jambo kali, binadamu tagundua.

Ujuaji jua kali, mambo mengi gharimia,
Ujuaji lokidhili, biasharayo tafumua,
Ujuaji hutufeli, masikini kutujia,
Ujuaji jambo kali, binadamu tagundua.

Ujuaji tena ghali, mambo mengi unaua,
Ujuaji wafadhili, misa'da kudidimia,
Ujuaji kila hali, hupati kusisimua,
Ujuaji jambo kali, binadamu
tagundua.

Ujuaji hawajali, kukwambiya solijua,
Ujuaji takufeli, maishani 'tojijua,
Ujuaji si asali, ni mbaya tatambua,
Ujuaji jambo kali, binadamu
tagundua.

*Kutoka: Meja S. Bukachi (Uketo wa Fasihi, uk 120- 121)*

MASWALI

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (Alama 1)
b) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (Alama 2)
c) Mwandishi anasema kuwa ujuaji ni nini? (Alama 2)
d) Taja tamathali za lugha zilizotumika katika shairi hili. (Alama 2)
e) Fafanua uhuru wa ushairi alioutumia malenga. (Alama 4)
f) Weka shairi hili katika bahari mbalimbali. (Alama 3)
g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (Alama 4)
h) Vifungu vifuavyo vina maana gani katika shairi?
   i. Majitapa
   ii. Gudurua

FASIHI SIMULIZI

*Soma utungo ufatao kisha ujibu maswali*



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Ndimi Kisoi, dume la ukoo mtukufu
Ulojipambanua kwa mabingwa
Wchezaji hodari wa ngoma
Ndimi dume lililoingia nyanjani
Makoo yakatetema
Yakang'ang'ania, gozi kusakata name.

Kijiji kizima kilinijua
Wazee walinienzi
Wakamiminika kiamboni
Mabinti kunikabidhi.

*Kutoka: Assumpta K. Matei (Fani ya Fasihi Simulizi, uk 113)*

Maswali

(a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 2)
(b) Jinsia ya nafsi neni ni gani? (alama 2)
(c) Eleza sifa zozote nane za kipera hiki cha fasihi simulizi (alama nane)
(d) Fafanua umuhimu wa kipera ulichokitaja hapo juu katika jamii (alama 8)

MTIHANI 3

CHOZI LA HERI- A. MATEI

1. "Riwaya ya Chozi la Heri inaakisi uozo uliomo katika Jamii nyingi barani Afrika"
Thibitisha kauli hii kwa kurenjerea Riwaya (al 20)

TAMTHILIA KIGOGO (P. KEA)

2. "Do ! Do ! Simameni ! Simameni! leo kutanyesha mawe ! "
i. Eleza muktadha wa dondoo hili (al 4)
ii. Fafanua mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili (al 4)
iii. Huku ukitoa mifano jadili hoja sita zinazodhihirisha jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika Tamthilia ya kigogo (al 12)

3. Kwa kuirejerea Tamthilia ya Kigogo eleza jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya Majazi

HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

(A.Chokoko na D.Kayanda)

4. "Kwetu tunapigania mikono ielekee vinywani. Mzoea vya sahani, vya vigae haviwezii"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al 4)
b) Tambua tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili (al 2)
c) Fafanua sifa nne za msemaji (al 4)
d) Jadili maudhui ya utabaka ukirejerea hadithi husika (al 10)

5. Jadili maudhui ya usaliti katika hadithi;
a) Mapenzi ya kifaraurongo (al 10)
b) Mame Bakari (al 10)

USHAIRI

6. *Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali.*

Mungu naomba subira, subira nayo imani
Imani iliyo bora, bora hapa duniani
Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Hiani pamwe ukora wenye kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na ufidhulu
Ufidhuli wa kudhuri, kudhuri wangu muwili
Muwili hata kidari, kidari kuwa thakili Thakili
kisinawiri, kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele
Muwele wa hitilafu, hitilafi ya nduwele
Nduwele kutakilifu, kutakilifu milele Milele
kutoniafu, kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vitomele vikwato
Vikwato pia maole, maole kufanya mito
Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto
Kitoto kilo vipele, vipele vyenye fiakuto.

Fukuto lanipa neno, neno hili kutamka
Kutamka wazi vino, vino subira kutaka
Kutaka imani mno, mno n'sipate wahaka
Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.

Mashaka haya ya leo, leo yawe yarnepita
Yaniepita na vilio, vilia vipishe nyota
Nyota njema ingarao, ing'arao kunikita
Kunikita salamani, salamani nikadata.

*a)* Kwa nini nafsi neni inaomba subira na amani ? (alama 2)
*b)* Shairi hili ni la Bahari gani kwa kuzingatia : (alama 4)
i) Mpangilio wa maneno
ii) Mpangilio wa vina
c) Kwa kutokea mifano eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (alama 4)
d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)
e) Kwa kutolea mifano, eleza jinzi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa kutekeleza arudhi. (Alama 6)

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali. (alama 20)**
**Barabara.**

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili
Lakini



© 2019 RWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi.

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
Kuwa tayari kupanda na kushuka.‖

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka.

Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena? Hadi lini? Labda
amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!
Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendelee kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijikokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi
kabla. *(Timothy Arege)* <u>Maswali.</u>

(a) Taja na ueleze aina ya shairi hili. (alama 2)

(b) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

(c) Fafanua dhamira ya shairi hili. (alama 2)

(d) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (alama 3)

(i) Tanakali za sauti
(ii) Mbinu rejeshi (iii) Taswira

(e) Eleza umhimu wa maswali balagha katika shairi. (alama 2)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

(f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari.
(alama 4)
(g) Eleza matumizi ya mistari mishata katika shairi hili.
(alama 2)
(h) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi.
(alama 3)
(i) Kuruba
(ii) Siha
(iii) Machweo

FASIHI SIMULIZI

8. Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yaliyoulizwa.

Hapo zamani za kale, Mungu alituma wajumbe wawili waende duniani. Wajumbe hawa ni Kinyonga na Mjusi. Kwanza alimtuma Kinyonga na kumwagiza akaseme "wanadamu hamtakufa." Kinyonga aliendа kwa mwendo wa kuduwaa, akasimama hapa na pale akila matunda ya miti. Kwa sababu ya hali hii alichelewa sana kufikisha ujumbe kwa binadamu.

Baada ya muda kupita, Mungu alimtuma Mjusi na ujumbe akaseme, "Mwanadamu sharti kufa." Mjusi aliunyanyua mkia akafyatuka pu! Mbio akawahi duniani kabla ya kinyonga kuwasili. Kwa haraka alitangaza agizo kuu, "Wanadamu sharti kufa!" Akarejelea haraka kwa Mungu. Baada ya muda kinyonga naye akafika duniana na kutangaza, "Wanadamu hamtakufa!" Wanadamu wakapinga mara na kusema, "La! Tumeshapata ujumbe wa Mjusi, wanadamu sharti kufa! Hatuwezi kupokea tena neno lako! Basi kulingana na neno la mjusi, wanadamu hufa.

a)

i.Tambua aina hii ya hadithi (al 2)
ii.Toa sababu za jibu lako katika (a) i. (al 1)

b) Eleza sifa tatu zinazohusishwa na ngano za fasihi simulizi katika hadithi hii. (al 3)
c) Fafanua hulka mbili za Kinyonga kwa mujibu wa makala haya (al 2)
d) Hadithi hii ina umuhimu gani? (al 4)
e) Taja njia zozote nne za kukusanya kazi za fasihi simulizi (al 4)
f) Fafanua jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza fasihi simulizi (al 4)

MTIHANI 4

CHOZI LA HERI ASSUMPTA MATEI

'Huyu ambaye mama alimwona kuwa gae, kumbe sasa ndiye chombo cha kunivusha bahari hii ya dhiki?'

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)
(b) Eleza sifa sita za mzungumzaji wa maneno haya. (Alama 6)
(c) Onyesha jinsi wahusika mbalimbali katika riwaya ya chozi la Heri walivyopitia 'bahari ya dhiki'.(Alama 10)

TAMTHILIA Kigogo – Pauline Keya.



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

'Nimekuja kuwakomboa sio kuwaumbua'.

(I)Eleza umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya. (Alama 8)

(II) Kwa kutumia hoja kumi na mbili, thibitisha kuwa mnenewa na wenzake walistahili kukombolewa. (Alama 12)

(3)'Acha porojo zako' Kigogo hachezewi;watafuta maangamizi!'

(I)Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)

(II)Fafanua sifa sita za kigogo anayerejelea. (Alama 6)

(III) Eleza mbinu kumi zilizotumiwa na kigogo kuonyesha 'hachezewi' (Alama 10)

HADITHI FUPI – Alifa chokocho na Dumu kayanda.

'Leo mwalimu mkuu atajua kwamba mdharao biu hubiuka'

(a)Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)

(b)Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika mktadha huu. (Alama 6)

(c)Eleza wasifu wa mzungumzaji wa maneno haya. (Alama 2)

(d)Jadili maudhui ya elimu kama yanavyojitokeza katika hadithi hii. (Alama 8)

(5)'Kusema kweli lakini hata mimi sikuwa na nadhari katika kumpenda msichana huyu … Nilimpenda kufa! Lakini! Kwao bure tu!'

(a) Eleza mkutadha huu. (Alama 4)

(b)Taja mtindo wa lugha uliotumika katika mkutadha huu. Alama 4

(c) Taja sifa mbili za mzungumzaji. (Alama 2)

(d) Onyesha maudhui ya umaskini katika hadithi fupi ya Ndoto ya mashaka.

USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Daima alfajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu;
Ni miti yote hujipinda migongo
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua

Akichekelea ha ha ha ha ha ha ha …
Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho;
Kuna jambo gani linamridhisha?
Kama si kujua ni kutokujua
Laiti angalijua, laiti angalijua!

**MASWALI**

(a)Eleza matatizo manne yanayompata mzungumziwa. (Alama 4)
(b)Eleza mtindo wa lugha uliotumiwa na mshairi na utoe mifano. (Alama 8)
(c)Taja nafsineni katika shairi hili. (Alama 1)
(d)Eleza toni ya shairi hili. (Alama 1 )
(e)Taja mbinu mbili za uhuru wa kishairi uliotumika na utoe mifano.
( Alama 2) (f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

**(7)Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili

Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ila ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili.



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Vingekuwepop viraka, kuutia, ngeushuruti mwili
Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili
Upya ukaungilika, kuvutia, roho na wake mwili.

Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
Sihofu kupata mawi, sitajua, kupigania mwili
Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili.

Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika, damu, jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili.

(a)Liweke shairi hili katika bahari tatu. (Alama 3)
(b)Eleza dhamira ya mshairi. (Alama 2)
(c) Eleza muundo wa shairi hili. (Alama 4)
(d) Toa mifano ya uhuru wa kishairi uliotumika. ( Alama 4)
(e)Eleza kwa kifupi maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (Alama 3)
(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

SEHEMU D

FASIHI SIMULIZI

A(i) Miviga ni nini? (Alama 2)
(ii) Eleza sifa nane za miviga. (Alama 8)
B (i) Ulumbi ni nini? (Alama 2)
(ii)Eleza sifa nane za ulumbi (Alama 8) MTIHANI 5

SEHEMU YA A: HADITHI FUPI

Alifa chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba

1. <u>Lazima</u>

"Doa ndio kawaida inayobainisha maisha ya mwanadamu."Onyesha ukweli wa kauli hii kwa mujibu wa hadithi za: Shogake Dada ana Ndevu, Mame Bakari, Shibe Inatumaliza na Mtihani wa Maisha. (alama 20)

SEHEMU YA B: RIWAYA

*Assumpta Matei: <u>Chozi la Heri</u>*

Jibu swali la 2 au la 3

2. Alijiona kama mfa maji ambaye anakabiliwa na mtutumo wa mawimbi ya misiba, mmoja baada ya mwingine.

(a) Bainisha muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Eleza sifa tatu za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 3)
(c) Eleza tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
(d) Fafanua masaibu yaliyomkumba mrejelewa. (alama 3)
(e) Huku ukitolea mifano riwayani, jadili matatizo yanayowakumba wanajamii katika ndo (alama 8)

3. Eleza ufaafu wa anwani Chozi la Heri. (alama 20)

SEHEMU YA C: TAMTHILIA



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851706)

Pauline Kea: Kigogo

4. "Hivi vishahada vyao wanavyovipata siku hizi vinawavimbisha vichwa!"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Taja tamathali zozote mbili zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

(c) Eleza changamoto zilizomkabili mrejelewa na wenzake. (alama 14)

5. Mwandishi wa Kigogo amefanikiwa sana katika matumizi yake ya mbinu ya jazanda na kinaya. Fafanua ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia. (alama 20)

SEHEMU YA D: USHAIRI

6. Ipo Siku

Jua la mashariki limezibwa
Na machweo ya magharibi
Tukabaki kuhesabu siku
Na kila sekunde inayopita
Ikilifyatua shaka jipya
Ambalo bado kidogo
Litakuwa limeliua tumaini Na
sumu yake kulipuka hadharani
Ulimwengu ushuhudie.

Ni upeo wa sayansi:
Waundapo silaha
Mabomu ya masafa ya mbali
Yanayomwaya yake mimweso
Na kutudonoa
Kama yule jogoo
Wa radi.

Ni upeo wa uhayawani:
Tuundapo silaha
Mabomu ya masafa ya karibu
Au zana za kukingia wao jogoo
Asitudonoe na kututia mautini
Katika yetu ardhi
Walipoishi na kuzikwa wetu wahenga.

Ni udikteta sisi kuongozana vibaya
Ni udikteta viongozi kuwaua wapinzani
Ni unyama watu kupigwa risasi
Ni unyama wananchi kuteswa
Lakini
Ni demokrasia wao kutuvamia
Na yetu ardhi kukalia
Ni demokrasia kuwaua viongozi wetu
Pamoja na wananchi kwa yao



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

makombora Yenye kiu ya damu yetu.

Ni haki kutukatia mifereji ya maji
Tukanyauka na kujifia kama vipando
Katika majira magumu ya ukame?
Ni utu kuwatesa watoto wetu
Waliojisabilia kuipigania nchi katika ushinde
Katika ardhi hii tulopawa
Naye Mola Moliwa?

Lakini fahamuni:
Tofauti kati ya hadithi fupi na ndefu
Ni kuwa ndefu huchukua mrefu wakati kuisha
Na ile fupi huchukua muda mfupi
Zote lakini zina miisho
Na hii nayo ipo siku
Ukingoni itafika
Hatimaye watoto wetu wapate tena
Jioni kuitamani
Jioni isiyo na mimweso
Mimweso ya kutishia wao
uhai Na mingurumo na
mirindimo Ya kutangaza yao
maangamizo!

Najua sitokuwepo hili kushuhudia
Lakini kwangu itakuwa si kitu
Muhimu ni wajukuu wafahamishwe
Kuwa hapa nilipita na kushuhudia
Binadamu akiutekeleza unyama
Alioupindua juu chini, nje
ndani Kama funzo la
demokrasia Kwa ulimwengu
kipofu!

<u>Maswali</u>

(a) Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)
(b) Taja na kueleza nafsi – neni katika shairi hili. (alama 2) (c) Jadili matumizi ya mbinu zifuatazo katika shairi hili.
(i) Kinaya (alama 3)
(ii)Usambamba (alama 3)
(iii)Jazanda (alama 3)
(d) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 4)



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724251706)

(e) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

INSANI TWAJILAANI

Ya wapi silika hino, ya kwenda kinyumenyume?
Nilijibu hata kwa wino, majibuyo niyasome,
Kuno 'geuza maneno, na kuyafanya maleme,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Insiya jilaani, ni bora wazi niseme,
Kukubalia idhini, mimba wakazikateme,
Hiyo nayo haki gani, wasiyoona mit ume,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Twajilaani laana, kijitakia ujume,
Nayo habari hatuna, twajiletea ukame,
Pia habari hatuna, ni wana sio vimeme,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Muswada siyo halali, wakuviavya vikembe,
Utawapea halali, mabinti wetu watambe,
Magulamu ja fahali, nao wakame pembe,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

Kuavya mimba ni dhambi, ya kumuudhi Rahimu,
Laana twajaza tumbi, ya moto wa
jahanamu, Tuache vino vitimbi,turudie
utimamu, Haramu kuwa halali, insani
twajilani.

Jambo hili nawambia, litazidisha ukware,
Ni ya uvundo tabia, ni afueni tuisare,
Tuweze kuitubia, tuwache zino parare,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.
Muida ndio sinao, nina mengi ya kusema,
Wapigania hakio, zingatia nayosema,
'sipashe mswada huo , ni madhambi ya kuchoma,
Haramu kuwa halali insani twajilani.

MASWALI

a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama 1)
b) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)
c) Kwa kutolea maelezo mwafaka,tambua bahari tatu katika shairi hili (alama 3)
d) Eleza tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika shairi na utolee ithibati (alama 2)
e) Onyesha jinsi idhini ya mtunzi ilivyotumika kutimiza arudhi katika shairi hili (alama 4)
f) Bainisha toni ya shairi hili (alama 1)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

g) Tambua maudhui mawili yanayotawala shairi hili (alama 2)
h) Tambua madhara matatu ya uavyaji mimba ( alama 3)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

7. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mtu A: Tulienda kwa hiyo sherehe jana…
Mtu B: Ooh! Kumbe ulipata ngiri mbili za kiingilio?
Mtu A: Nilivaa chupa woiyee!
Mtu B: Ulimuona yule kijana Kamba?
Mtu A: Hehehe! Yule huringa mbaya…
Mtu B: Huyo alitoka mbio aliposikia kumethuka…

<u>Maswali</u>

(a) Tambua kipera cha utanzu wa semi kinachohusishwa na kifungu hiki. (alama 1)
(b) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. (alama 5)
(c) Ngomezi ni nini? (alama 2)
(d) Jadili sababu ambazo zimesababisha kuzorota kwa matumizi ya ngomezi katika jamii ya kisasa. (alama 6)
(e) Jadili sifa za sogora zinazojitokeza nyanjani wakati wa utafiti. (alama 6)

MTIHANI 6

SEHEMU A: SWALI LA LAZIMA:

1 '' Alikumbuka jinsi rafiki yake…alivyofishwa kwa njia hii.akili yake ilimtambia kisa chenyewe kana kwamba inataka kumwonya.''

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizojitokeza kwenye dondoo hili (alama 4)
(c) Tathmini nafasi ya anayelengwa katika kauli hii kuijenga riwaya hii (alama 12)

SEHEMU B: TAMTHILIA: KIGOGO (Pauline Kea)

2. Eleza matakwa kumi ya wanasagamoyo.(alama 20)
3. 'Dalili ya mvua ni mawingu, lazima tuwe macho'
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili.(alama 4)
   b) Bainisha tamathali mbili za lugha katika dondoo.(alama 2)
   c) Eleza sifa nne na umuhimu wa mzungumziwa.(alama 6)
   d) Eleza kwa ufafanuzi kauli kuwa majina ya wahusika katika dondoo ni majazi. (al.4)

SEHEMU C: HADITHI FUPI (Tumbo Lisiloshiba Na Hadithi Nyingine)

4. Eleza sifa na umuhimu wa wahusika wafuatao.
   a) Dadi
   b) Kidawa
5. Eleza changamoto zinazoikumba asasi ya ndoa ukirejelea hadithi ya Masharti ya Kisasa.



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851706)

SEHEMU D:  USHAIRI

6, Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Naingia ukumbini, nyote kuwakariria,
Ushairi niwapeni, hoja nitawaachia,
Mnipe masikioni, shike nachoelezia,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Naanza kwa uzalendo, nchi yetu tuipende,
Yadhihirishe matendo, nchi yetu tuilinde,
Wa kila mtu mwendo, usije kawa mpinde,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili

Wote tuwe na umoja, tuuache ukabila
Kabila lisiwe hoja, mwenza kumnyima hela,
Taifa letu ni moja, Mkenya ndilo kabila,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Linda demokrasia, uongozi tushiriki,
Haki kujielezea, wachotaka na hutaki.
Changu naweza tetea, demokrasia
haki,  Taifa sio taifa, pasi kuwa
maadili.

Tena adili usawa, mgao raslimali,
Bajeti inapogawa, isawazishe ratili.
Idara zilizoundwa, _faidi kila mahali,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Tuwe na uadilifu, twache tamaa ya hongo,
Tusiwe na udhaifu, wa kuwa watu waongo,
Tukomeshe uhalifu, kisha tuache maringo,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Ubinafsi si adili, ila ni kusaidia,
Ukiwa nayo mali, asiyenacho patia,
Kama mtu mswahili, ubinafsi achia,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Na inavyoelezea, katiba ni kielezi,
Tutii kwa mazoea, hadi kijacho kizazi,
Kwa hayo nitamwachia. hiyo ya ziada kazi,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851706)

a) Eleza mambo yoyote manne ambayo mshairi anashauri taifalifanye ili kuwa na aadili. (alama 4)
b) Taja tamathali yoyote moja inayojitokeza katika shairi hili. (alama 2)
c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia kigezo kifuatacho: (alama 1)

*Mpangilio wa vina*

d) Bainisha nafsineni (mzungumzaji) katika shairi hili. (alama 2)
e) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
f) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa nne (alama 4)
g) Andika ubeti wa pili kw lugha nathari (alama 4)
h) Eleza maana ya nene lifuatalo kama ilivyotumiwa katika shairi: (alama 1)
i) hongo

7. Soma shairi ifuatalo kisha ujibu maswali.

Jana ilikuwepo, ikapita
Kwenye giza la sahau
Jana ilipiga kuathiri
Athari ijayo leo
Leo tunajua kesho tunaibashiria

Kesho ipapo na hatuijui
Kesho, itapiga au itapuliza?
Au itapita pasi na chochote
Kama moshi usio mashiko?

Kesho hatuioni Lakini yaja ...
Twaihisi Twaihisi Twaihisi
Ipo,
Yajongea
Hiyo na taathira zake
Inakuja
Yasogea
Yaja mbio
Yafikia upeo unaoitwa leo
Basi kumbuka
Maisha ni ubishi, yakabili!
Maisha ni jasiri, jusurisha!
Maisha ni huzuni, yashinde!
Maisha ni msiba, uweze!

Maisha ni wajibu, tekeleza!
Maisha ni ni fumbo, liague!
Maisha ni tatizo, litatue!
Maisha ni ahadi, itemize!



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Maisha mapambano, wana nayo!
Maisha ni zawadi, ipokee!
Maisha ni mchezo, uxhezee!
Maisha ni nyimbo, iimbe!
Maisha ni fursa, itumie?
Maisha ni ureda, furahia!
Maisha maumbile, changamkie!
Maisha ni lengo, lifike!
Maisha ni mwendo, yaendee!
Maisha ni uzuri, ustarehee!
Maisha liwazo, yapumzikie!

(a) Lipe kichwa mwafaka shairi hili. (alama 2)
(b) Fafanua maudhui ya shairi hili. (alama 6)
(c) Onyesha muundo wa shairi hili. (alama 4)
(d) Taja na ueleze tamathali tatu za usemi alizotumia mwandishi wa shairi hili. (alama 6)
(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumia katika shairi. (alama 2) Twaimaizi Yajongea

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**i) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Mtu mmoja alimpa mke wake nambari yake ya simu. Kila mara bibi akipigia mumewe simu, ilipokelewa na sauti nyororo —mteja wa nambari uliopiga hapatikani kwa sasa. Alifunga safari kumtembelea mume wake mjini na kukabiliana na huyu kisura.

MASWALI

a) Bainisha kipera cha utungo huu. (Alama.2)
b) Onyesha sifa tano za kipera hiki. (Alama.5)
c) Eleza manufaa matano ya kipera hiki. (Alama.5) ii) Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali:

<u>Ewe mpwa wangu</u>,
Kwetu hakuna mwoga,
usiwe kama msichana,
Uoga ukikufika,
huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tulichinja
ili uwe mwanamume
Iwapo utatingiza kichwa
Uhamie kwa wasiokatwa
Waume wa mbari yetu
Si waoga wa kisu Wao
hukatwa kuanzia macheo
hadi machweo.
Simama jicho liwe juu



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Ngariba alilala jikoni
Visu ametia makali
Kabiliana na kisu kikali
Wengi wasema ni kikali
Mbuzi utampata
Na hata shamba la mahindi
Usiende kwa wasiotahiri.

MASWALI

(a) Huu ni wimbo gani? Fafanua (Alama.2)

( (b) Eleza shughuli mbili za kiuchumi zinazodokezwa na wimbo huu. (Alama.2) (c) Onyesha taasubi ya kiume inavyojitokeza katika wimbo huu. (Alama.4)

## SEHEMU YA PILI

### MTIHANI WA 1

SHAIRI -SWALI LA LAZIMA

1. M.S.Khatib:*Fungate ya Uhuru*

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata**

Maendeleo ya umma
Sio vitu maghalani
Kama tele vimesaki
Lakini havishikiki
Ama havikamatiki
Ni kama jinga la moto
Bei juu

Maendeleo ya umma
Sio vitu gulioni
Kuviona madukani
Kuvishika mikononi
Na huku wavitamani
Kama tamaa ya fisi
Kuvipata ng'o



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351796)

Maendeleo ya umma
Sio vitu shubakani
Dhiki ni kwa mafakiri
Nafuu kwa matajiri
Ni wao tu washitiri
Huo ni ustiimari
Lo! Warudia
Maendeleo ya umma
Ni vitu kumilikiwa
Na wanyonge kupatiwa
Kwa bei kuzingatiwa
Bila ya kudhulumiwa
Na hata kuhadaiwa
Hiyo ni haki

Maendeleo ya umma
Dola kudhibiti vitu
Vijapo nchini mwetu
Na kuwauzia watu
Toka nguo na supatu
Pasibakishwe na kitu
Huo usawa

Maendeleo ya umma
Watu kuwa na kauli
Katika zao shughuli
Vikaoni kujadili
Na mwisho kuyakubali
Maamuzi halali
Udikteta la


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Maendeleo ya umma

Watu kuwa waungwana

Vijakazi na watwana

Nchini kuwa hakuna

Wote kuheshimiwa

Wazee hata vijana

Maswali

a) Huku ukitoa mifano, toa ithibati kuwa hili ni shairi huru (alama 5)
b) Mtunzi wa shairi hili alidhamiria nini? (alama 1)
c) Bainisha matumizi mawili ya tamathali za usemi katika shairi hili. (alama 2)
d) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya kawaida (alama 4)
e) Eleza mambo yanayodhihirisha kuwa nchi imepiga hatua kiuchumi kwa mujibu wa shairi hili. (alama 4)
f) Eleza kwa kutoa mfano mbinu ambayo mtunzi wa shairi hili ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa sita. (alama 2)
g) Eleza aina ya urudiaji unaojitokeza katika ubeti wa pili na uonyeshe umuhimu wake katika shairi hili. (alama 2)

## RIWAYA

Assumpta K. Matei: c*hozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2. Riwaya ya *Chozi la Heri* inasawiri adha zinayozikumba nchi za Kiafrika. Thibitisha kwa kutoa mifano mwafaka. (alama 20)

3. "Vijana hawapaswi kungojea kufanyiwa kila kitu. Tumewapa nyavu za kuvulia, nao wanaona wangoje kuletewa samaki!"

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Fafanua maudhui yanayodhihirika katika dondoo hili (alama 2)
   c) Tambua na ueleze mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 4)
   d) Eleza maafa yaliyomwandama msemaji wa kauli hizi (alama 4)
   e) Taja na ueleze sifa sita za msemewa (alama 6)

## TAMTHILIA

P. Kea: *Kigogo*

*Jibu swali la 4 au la 5*

4. Tamthilia ya *Kigogo* imesheheni mambo ya kukatisha tamaa. Thibitisha huku ukitoa mifano inayofaa.



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

(alama 20)

5. "Walikuwa wanataka kukukanganya tu ili usiweze hata kuwakisia waliokudhuru"

   a) Eleza umuhimu wa msemaji katika dondoo hili (alama 4)
   b) Ni maudhui yapi yanayodhihirika katika dondoo hili? (alama 2)
   c) Msemewa na wenzake ambao wanapigania ukombozi pamoja walikumbana na vizingiti anuai. Eleza kwa kutoa
   mifano (alama 14)

## HADITHI FUPI

A.Chokocho na D. Kayanda: *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au la 7.*

*Ali A. Ali: Ndoto ya Mashaka*

6. "Na kwa nini hazitaki kuukemea mfumo huu wa maisha? Mfumo wa mwenye nacho kuendelea kupata na msinacho
   kuendelea kukosa?"

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Fafanua maudhui mawili yanayodhihirika katika dondoo hili (alama 4)
   c) Tambua na ueleze sifa sita za msemaji (alama 6)
   d) Eleza athari ya "msinacho kuendelea kukosa" katika jamii husika (alama 6)

7. Fafanua jinsi suala la elimu limeshughulikiwa katika *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* kwa kurejelea hadidhi zifuatazo:
   a) *Mapenzi ya Kifaurongo* (alama 5)
   b) *Shogake Dada ana Ndevu* (alama 5)
   c) *Mtihani wa Maisha* (alama 5)
   d) *Mwalimu Mstaafu* (alama 5)

## FASIHI SIMULIZI

8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali

   Hapo zamani za kale paliishi mtoto katika kisima kimoja. Siku moja mtoto huyu aliokota kijiwe karibu na soko kuu. Kijiwe kilikuwa kikimeremeta kwa rangi mbalimbali na kilizingirwa na pete ya dhahabu.

   Mtoto huyu na wenzake walianza kurushiana kijiwe hicho. Baada ya muda kilianza kuongezeka umbo na kuonekana kama kiwiliwili cha binadamu. Kikaanza kuwakimbiza wale watoto. Kutokana na ukelele wao, watu walikuja kutazama nini kilikuwa cha mno. Walipofika walikutana ana kwa ana na dubwana hilo. Lilizidi kuongezeka umbo na likawameza wote pamoja na mifugo wao. Wachache waliojaribu kukimbia liliwashika kwa mikono yake mipana na mirefu. Kwa bahati njema alikuwepo mama mmoja



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

aliyeona hayo yote. Alikuwa mbali kiasi na hapo. Aliteremka kutoka kilele cha mlima na kuwapata wakulima makondeni na sawia akawajuza kuhusu kitendo kilichomwogofya sana. Wote wakaacha shughuli zao na wakatwaa silaha zao wakaelekea soko kuu.

Dude sasa lilikuwa limejilaza baada ya shibe, wakulima wale walichagua watu sita ambao walijulikana kwa ushujaa wao. Pamoja walilinyemelea lile nyangarika na kulikata mara moja. Lilitoa mkoromo mkuu kabla halijakata kamba. Punde, wanakijiji kwa uangalifu mkubwa walitoboa tumbo lake wakitarajia kupata maiti za wapenzi wao pamoja na mifugo wao. Wote walijawa na furaha kuu walipoona wapenzi wao wakijichomoza kutoka tumboni, mmoja baada ya mwingine hadi akatoka yule wa mwisho. Mbuzi, kondoo na ng'ombe wote walitoka mmoja mmoja. Siku hiyo kuliandaliwa sherehe ya kumshukuru Muumba kwa wema wake. Watoto walishauriwa wasithubutu kuchezea vitu wasivyovijua.

**Maswali**

a) Ainisha kipera hiki cha hadithi (alama 1)
b) Fafanua mambo manne yanayodhihirisha kuwa kipera hiki ni sanaa. (alama 4)
c) Mwasilishaji bora wa kipera hiki anafaa kuwa na sifa gani? Eleza zozote nne. (alama 4)
d) Onyesha mifano miwili ya fantasia katika hadithi hii. (alama 2)
e) Eleza majukumu manne ya tungo hizi kwa wanajamii (alama 4)
f) Eleza majukumu matano ya mtindo uliotumiwa kuanzisha hadithi hii. (alama 5)

## MTIHANI WA 2

### SEHEMU A: TAMTHILIA

P. Kea: *Kigogo*

1. Lazima

Chombo chenye rubani imara huhimili vishindo na hasira ya mawimbi makali.

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b. Tambua na ufafanue fani iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
c. Onyesha jinsi msemewa alivyofeli kuhimili 'vishindo na hasira ya mawimbi makali' katika tamthilia hii. (alama 4)
d. Eleza kwa tafsili mambo yoyote **kumi** yanayokwaza usawa katika jamii ya *Kigogo*. (alama 10)

### SEHEMU B: USHAIRI

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.* Ewe hisia!

Umeniamshia ndoto niloisahau zamani
nyimbo ya kale
na mdundo usonivutia ila
hayawani na mwangu rohoni.


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Tulia sasa tulia
Hebu tulia ewe hisia ulo mtimani
Nataka katu kusisimka kwa sauti yako laini
Kwani njia zetu ni daima hazioani

Umesubutu vipi kuniita kutoka mwako ngomeni
ulimosahauliwa tangu zamani
Basi yawache maombolezi yako yaso maoni,
yawateke hao mashujaa wa kale
wafu walo kaburini.

Hebu tulia, usiniingilie
Usinihangaishe!
Kukuandama katu haimkini
Kwani hata sasa…kwa kukuwaza tu dakika hini
naona majuto ya mbali moyoni
kama kwamba nimegawa wangu wakati na wazimu, majinuni.
Basi nenda zako hisia…shuu…hebu tokomea.

Maswali

(a) Huu ni utungo wa aina gani? (alama 2)

(b) Huku ukitoa mifano, fafanua sifa zinazoufanya utungo huu kuwa shairi (alama 5)

(c) Mistari mishata ni nini? Toa mifano kwenye shairi hili. (alama 4)

(d) Fafanua tamathali za kifasihi katika shairi hili. (alama 3)

(e) Eleza mbinu **tatu** alizotumia mtunzi kutosheleza kaida za kishairi. (alama 6)

3. *Soma shairi lifwatalo kisha uyajibu maswali yanayoliandama:*

Naandika yangu haya, kwa uwezo wa Wadudi,
Kanipa njema afiya, kumsifu sina budi,
Nifundishie insiya, hino methali ya jadi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo

Ago mchama huuya, mbele mambo yakizidi,
Hurudi pakawa kaya, kupapenda hana budi,
Kwingi angawayawaya, ago shuruti arudi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI [illegible])

Kule kwetu Mwarakaya, kijiji chetu cha jadi,
Yalidhihirika haya, bwana mmmoja mkaidi,
Aloalikwa ulaya, kadhani ‘mepata sudi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo,

Alidhani hatauya, ‘endapo nchi *baidi*,
Na kusema bila haya, kwa inda na ukaidi,
Kwamba akenda ulaya, harudi kwenya samadi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Aliranda akitaya, kwa mbwembwe na zake tadi,
Nguo moto kazitiya, nyumbaye akainadi,
Kasema vyote ‘ishiya; kurudi sina ahadi
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Matusi aliyamwaya, mengi yasiyo idadi,
Mkewe kamwita yaya, na kudharau abidi,
Kanena *‘mekata waya’*, ng’ambo nenda kufaidi,
Mchama ago hayeli, huenda akauya papo,

Ng’ambo alielekeya, kwa vishindo kama radi,
Kumbe aliyemwendeya, kabambwa kwa ufisadi,
Vya watu amebugiya, rushwa na kuhepa kodi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Kombo yakamwendeya, mambo mno yakazidi,
Akabakia kuliya, nyumbani ataka rudi,
Nyumba ipi ‘taingiya’, hana tena tabaradi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo

*Maswali*

a) *Kwa kutolea ushahidi ufaao shairini, jadili kifupi maswala* **matatu** *makuu ambayo mtunzi ameyashughulikia.* (alama 6)

b) *“Mtunzi huyu ni bingwa wa kutumia lugha kupitisha ujumbe.” Tetea.* (alama 4)

c) *Fasiri ujumbe wa mtunzi katika ubeti wa* ***sita****.* (alama 4)

d) *Nafsi nenewa katika shairi hili ni nani? Thibitisha.* (alama 2)

e) *Zaidi ya tarbia, ungelipangaje tena shairi hili?* (alama 2)

f) *Fafanua msamiati ufwatao kama ulivyotumika shairini*: (alama 2)

i. *Baidi* ii. *‘mekata waya’*



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

*Jibu swali la 4 au la 5*

A. Chokocho na D. Kayanda: *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

4. "Madhila ya mtoto mvulana katika karne ya ishirini na moja ni mengi." Tetea kauli hii kwa hoja ishirini ukirejelea hadithi ya *Mapenzi ya Kifaurongo*, *Masharti ya Kisasa* na *Ndoto ya Mashaka*. (alama 20)

5. Salma Omar: *Shibe Inatumaliza*

(a) " Sijali lawama mnonilaumu"

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) DJ na wenzake wanaonekana kufurahia maudhui ya wimbo huu. Thibitisha. (alama 6) (b)

Alifa Chokocho: *Shogake Dada ana Ndevu*

"…tumshukuru kwa jinsi alivyomwongoza na kumwelekeza kwenye njia iliyonyooka" Ukirejelea wasifu wa Safia, tetea na upinge kauli hii. (alama 10)

## SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

6. "Magwiji wa uwanda mpana wa tamaduni za Kiafrika: wazee walioila chumvi wakabobea katika falsafa za turathi zetu, maghuluma wenye misuli tinginya na vifua vya mfumbata vinavyostahimili hujuma za kila nui na malaika wa kike uliosheheni mizinga na chemichemi ya urembo, nawasabahi. Wa zamani waliamba kuwa mwacha mila ni mtuma. Turathi zetu ni uhai. Turathi zetu ni msingi wa ubinadamu wetu. Turathi zetu zinabeba mustakabali wetu. Tuzienzi kama tuenzivyo asali."

Maswali

(a) (i) Tambua kipera cha utanzu wa mazungumzo kinachohusishwa na kifungu hiki. (alama 1)

(ii) Thibitisha jibu lako katika (i) kwa mifano yoyote **mitatu**. (alama 3)

(b) Iwapo umehudhuria utendaji wa kipera hiki nyanjani eleza sifa **tano** za mtendaji utakazoziona zisizojitokeza kwenye kifungu. (alama 5)

(c) Taja na kueleza miktadha **minne** ambamo kipera hiki kinaweza kutumiwa katika jamii ya kisasa. (alama 4)

(d) Andika sifa zozote **nne** za jamii ya nafsi neni katika utungo huu. (alama 4 )

(e) Eleza njia **tatu** za ukusanyaji wa data unazoweza kutumia kukusanya data kuhusu kipera hiki. (alama 3)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

SEHEMU YA E: RIWAYA

A. Matei: *Chozi la Heri*

*Jibu swali la 7 au la 8*

7. "Nitapigana kwa jino na ukucha kuulinda utu wangu."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Eleza umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (alama 4)

(c) Kwa kutolea mifano riwayani, thibitisha namna binadamu alivyopungukiwa na utu.

(alama 12)

8. Mwanamke ametwezwa katika kiwango sawa na namna alivyotukuzwa. Thibitisha ukweli wa madai haya kwa kurejelea riwaya ya *Chozi la Heri.* (alama 20)

MTIHANI WA 3

*SEHEMU YA A: RIWAYA*
*Assumpata K. Matei: Chozi la Heri*

*LAZIMA*

1. "Haiwezekani! Hili haliwekazi! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Eleza kwa kifupi yaliyowapata wahafidhina baada ya usemi huu. (alama.4)

(c) Riwaya ya chozi la heri inaonyesha maovu yanayotamalaki katika jamii.Thibitisha. (alama 12)

SEHEMU B: TAMTHILIA *Kigogo.Pauline Kea.*

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. Tatizo la uongozi katika bara la Afrika ni kikwazo kikubwa cha maendeleo. Kwa kurejelea matukio kwenye tamthilia ya kigogo, jadili ukweli wa kauli hii (alama 20)

AU

3. "Mtalipa kila tone la damu mlilomwaga sagamoyo ;wewe na watu wako."



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851706)

a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)

(c) Eleza sifa za mzungumzaji (alama 4)

(b) Thibitisha kwa kutoa mifano kuwa maisha ya anayezungumziwa yametawaliwa na dhuluma.

(alama 12)

*SEHEMU YA C: HADITHI FUPI*

4. Kwa kurejelea hadithi ya mapenzi ya kifaurongo, onyesha jinsi jamii imegawanyika kitabaka kuegemea. i. Kielimu ii. Kikazi

iii. Kiuchumi (alama 20)

*SEHEMU D: SHAIRI* <u>WASIA</u>

5. Huno wakati mufti, vijana nawausia
Msije juta laiti, mkamba sikuwambia
Si hayati si mamati, vijana hino dunia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula

Japo aula kushufu, na machoni vyavutia
Dunia watu dhaifu, yaugua nasikia
Vijana nawasarifu, falau mkisikia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

Jepusheni na zinaa, mlale penye sheria
Msije andama baa, makaa kujipalia
Jepusheni na zinaa, madhara kukadiria
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia
Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia
Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia
Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Wawapi leo madume, anasa walopapia?
Wamepita ja umeme, leo yao sitoria
Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851796)

Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula

Nambie faida gani, nambie ipi fidia
Upatayo hatimani, waja wakikufukua
Ila kufa kama nyani, kasoro yako
mkia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula.

Vyatiririka tariri, vina vyanikubalia
Alo bora mshairi, pa tamu humalizia
Nahitimisha shairi, dua ninawapigia
Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Ewe Mola mtukuka, si shaka wanisikia
Wakingie wanarika, na anasa za dunia
Amina wangu Rabuka, dua yangu naishia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

<u>MASWALI:</u>

a) Ni ujumbe gani wanaopewa vijana kupitia shairi?. (alama 4)

b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. (alama 2)

c) Eleza bahari ya shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 2)

i)idadi ya vipande katika mshororo ii) mpangilio wa vina katika beti.

d) Eleza mbinu zozote mbili za kishairi zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)

e) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari (alama 4)

f) Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)

g) Tambua: (alama 2)
i) Nafsi neni ii)

Nafsi nenewa

h) Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo iliyotumika katika ubeti wa tano. (alama 2)

i) Eleza maana ya msamiati: 'aula' (alama 1)

*SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI*

6. a) Eleza maana ya miviga. (alama.2) b) Eleza sifa tano za miviga.



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851706)

(alama.5)

c) Miviga ina udhaifu gani. (alama.3)

d) Fafanua umuhimu wa ngomezi katika jamii. (alama.6)

e) Eleza vizingiti viwili vinavyokumba ngomezi. (alama.4)

## MTIHANI WA 4

1. SWALI LA LAZIMA

a) i) Semi ni nini? (alama 1) ii) Fafanua sifa nne za misimu (alama4)

b) Soma wimbo ufuatao kasha ujibu maswali

Ewe kilizi
Ulozo wea kujificha
Nyumaya mama kujikinga, dhidiyamilio
Yanadiilo juu mbinguni
Jua kesho ni siku ya siku
Siku ya kujua mbivu na mbichi
Kutofautisha jogoo na vipora
Naribatakapo shika, chake kisu
Ndipo utakapo jua bayana
Ukoo wetu si wakunguru
Ikiwa hutayari
Kisukuki dhihaki
sithubutu kamwe, wanja ni kuingia
sijekuniaibisha miye, amiyo naakrabanzima!

Maswali

i) Huu wimbo huitwaje? (alama1)

ii) Eleza majukumu yoyote manne yanayotekelezwa na wimbo huu katika jamii (alama4)

c) i) Mivigha ni nini? (alama2)

ii) Eleza sifa tatu za mivigha (alama 3)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

d) Fafanua matatizo matano ambayo yanaikumbwa fasihi simulizi duniani (alama5)

SEHEMU YA B

RIWARA: CHOZI LA HERI: ASUMPTA MATEI

2. "…haifai kucheza na uwezo wa vijana, waoni kama nanga. Huwezi kuzamisha nakuiongea merikebu."

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

   b) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizo tumika katika dondoo (alama 4)

   c) Kwa kurejelea riwaya hii, onyesha jinsi vijana wamezamisha merikebu yawa hafidhina (alama12)

3. Baada ya dhiki faraja. Onyesha vile ukweli wa methali hii unavyo dhihirika kwenye riwaya (alama20)

SEHEMU YA C

TAMTHILIA: KIGOGO: PAULINE KEA

4. "Sitaki kuaibishwa na mwanamke mimi, siwezi."

   a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

   b) Fafanua kwa hoja nane kuwa msemaji wa maneno haya anafaa kuaibishwa (alama16)

5. a) Jadili jinsi kumia mbazo kwazo maudhui ya ukatili yanajitokeza katika tamthilia ya Kigogo (alama10)

   b) Eleza mifano mitato ya matumizi ya kinaya katika tamthilia ya Kigogo (alama10)

SEHEMU YA D : HADITHI FUPI

TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

6. Eleza nafasi ya vijana katika jamii ukerejelea hadithi fupi zifuatazo.

   a) Mapenzi ya kifa urongo (alama 5)

   b) Shogake Dada anaDevu (alama 5)

   c) Mame Bakari (alama10)

7. Ndoto ya mashaka: Ali Abdalla Ali

   "Sasa nimechoka mja. Nimechoka hata naradua kufa kuliko kuishi. Hadilini haya mashaka ya



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

kutengenezwa? Mashaka ya mashaka!

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika (alama 4)

c) Fafanua mambo sita yanayomfanya mrejelewa aradue kufa. (alama12)

8. SEHEMU YA E: USHAIRI

*Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali*

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimecho katiki
Natamani kuketi
Ni'nyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini

Azmayani sukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinu konakuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi

Punde na tumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ilikupanda tena
Ghaflanakumbukailivyosema
Ile sauti zamani kidogo
"Kuwatayari kupanda na kushuka".



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351796)

Ingawa nimechoka
Jambo moja dhahiri
Lazima hufuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka

Jambo moja nakumbuka;
Mungu Je nimwombe
tena?Hadilini?
Labda amechoshwa na omba omba zangu
Nashangaa tena!
Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendelee kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijikokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa nakujinasua
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla.

***Maswali***

a) Taja naueleze aina ya shairi hili (alama 2)

b) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

c) Huku ukitoa mifano mwafaka eleza tamathali tatu za usemi ambazo zinajitokeza katika shairi (alama 3)

d) Mshairi ametumia uhuru wake wautunzi. Eleza mifano mitatu huku ukitolea mifano. (alama 3) e) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama 2)

f) Andika kifungu cha mwisho katika lugha ya nathari. (alama 4)

g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi (alama 4)
i) Kuruba ii)
Siha iii) Machweo
iv) Kujinasua


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

MTIHANI WA 5

SEHEMU A : RIWAYA – LAZIMA

1. Fafanua ufaafu wa anwani 'Chozi la Heri' (al. 20)

SEHEMU B TAMTHILIA YA KIGOGO

2. Uliona nini kwa huyo zebe wako ? Eti mapenzi!

i) Eleza muktadha wa dondoo. (al. 4)

ii) Andika mbinu za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili (al. 4) iii) Taja hulka za mnenaji unajitokeza katika dondoo. (al. 2)

iv) Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirekjelea tamthilia. (al. 10)

Au

3. Ni bayana kwamba viongozi wengi nchi zinazoendelea wamejawa na tama na ubinafsi. Thibitisha kaul hi ukirejelea tamthilia Kigogo (al. 20)

4.

SEHEMU C: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI ZINGINE

SHIBE INATUMALIZA

5. "Ndugu yangu kula kunatumaliza"

"Kunatumaliza au tunakumaliza"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)

b) Fafanua maana kitamathali katika kauli 'Kula tunakumaliza' (al. 10)

c) Kwa mujibu wa hadithi hii, kwa namna gani wasemaji wanadai kula kunawamaliza? (al.6)

Au

a) 'MAME BAKARI'

Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake, onyesha kwa mifano mwafaka. (al. 10)

b) 'MASHARTI YA KISASA'



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

"............... mapenzi ni mateso, ni utumwa, ni ukandamizaji, ni ushabiki usio na maana."

Thibitisha ukweli wa kauli hii kama unavyojitokeza kwenye hadithi. (al. 10)

<u>SEHEMU D : USHAIRI A</u>

6. MWANA

1. Kwani mamangu u ng'ombe, au u punda wa dobi ?
   Nakuuliza usambe, nayavunja madhehebi
   Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibabi
   Hebu nambie
   Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

MAMA

2. Nang'ona mwana nang'ona, sitafute angamiyo
   Sinipe kuja sonona, kwa uchungu na kiliyo
   Babayo mkali sana, kubwa pigo la babayo
   Kwani kelele kunena, huyataki maishayo ?
   Hilo nakwambia.

MWANA

3. Sitasakamwa. Kauli, nikaumiza umiyo Nikabeba idhilali, nikautweza na moyo
   Siuvuwati ukweli, hazidisha gugumiyo
   Baba hafanyi halali, huachi vumiliyo
   Hebu nambie.
   Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

   Nambie ipi sababu, ya pweke kwenda kondeni
   Nini yako matulubu, kulima hadi jioni ?
   Na jembe ukudhurubu, ukilitua guguni Yu
   wapi wako muhibu, Baba kwani simuoni?
   Hebu nambie.
   Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Baba kwani simuoni, kuelekea shambani?
Kutwa akaa nyumbani, na gumzo mitaani.
Hajali hakudhamini, wala haoni huzuni.
Mwisho wa haya ni nini ? ewew mama wa imani ?
Hebu nambie.
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Na kule kondeni kwako, ukate kuni kwa shoka
Ufunge mzigo wako, utosini kujitwika
Kwa haraka uje zako, chakula upate pika
Ukichelewa vituko, baba anakutandika
Hebu nambie.
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

Chakula kilicho ndani, ni jasho lako hakika
Kiishapo u mbioni, wapiti kupokapoka
Urudi nje mekoni, uanze kushughulika
Ukikosa kisirani, moto nyumbani wawaka
Hebu nambie.
Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo ?

MAMA
Wanitonesha kidonda, cha miaka na miaka
Usidhani nayapenda, madhila pia mashaka
Nakerwa na yake inda, na sasa nimeshachoka  Ninaanza kijipanga, kwa mapambano hakika
Hilo nakwambia

MASWALI

a) Mtunzi wa shairi hili alikuwa na dhaimira gani katika kutunga shairi hili (al. 2)
b) Shairi hili ni la aina gani. Toa ithibati (al. 2)
c) Yataje mambo yoyote matano anayolalamikia mwana (al. 5)


© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

d) Eleza kanuni zilizotumika kasarifu ubeti wa tatu (al.5)

e) Andika ubeti wa saba kwa lugha tutumbi (al. 4)

f) Eleza maana haya yaliyotumika katika shairi hili

i) Jaza (al. 1)

ii) Muhibu (al. 1)

7. <u>SHAIRI B</u>

Soma shairi hili kisaha ujibu maswali

1. Punda kalibebe gari, gari limebeba punda.
   Mwalimu ana pakari, muashi vyuma adunda
   Jaji gonga msumari, sonara osha vidonda
   Kinyume mbele.

2. Saramala ahubiti, muhunzi tiba apenda
   Mganga anabiri, baharini anakwenda
   Hata fundi wa magari, anatomea vibanda
   Kinyume mbele

3. Wakili anahiyari, biashara kuitenda
   Mtazame askari, akazakaza kitanda,
   Mkulima mashuhuri, jembe limemshinda
   Kinyume mbele

4. Apakasa daktari, ukili anaupinda Seveya
   kawa jabari, mawe anafundafunda, Hazini
   wa utajiri, mali yote aiponda,
   Kinyume mbele

5. Msemi huwa hasemi, wa inda hafanyi inda
   Fahali hawasimami, wanene walishakonda
   Walojitia utemi, maisha yamewavunda
   Kinyume mbele



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

6. Kiwapi cha kukadiri, twavuna shinda kwa shinda
   Tele haitakadiri, huvia tulivyopanda
   Mipango nmehajiri, la kunyooka hupinda
   Kinyume mbele

MASWALI

a) Mtunzi aliuwa na malengo gani alipotunga shairi hili? (al. 3)
b) Licha ya tarbia, eleza bahari nyingine zinazojitokeza katika shairi hili. (al. 4)
c) Eleza namna mtunzi alivyotumia uhuru wake. (al. 5)
d) Ni mbinu gani inayotawala shairi hili? (al. 2)
e) Uandike ubeti wa nne katika lugha nathari (al. 4)
f) Eleza toni ya shairi hili (al. 2)

## SEHEMU E

### 7. FASIHI SIMULIZI

1. Eleza vigozi vinne vya kuandika methali (al. 4)
2. Eleza fani zinazozijenga vitendawili vifuatavyo (al. 4)
   i) Ajenga ingawa hana mikono ii) Jani la mgomba laniambi habari zinazotoka ulimwenguni kotew
3. Nini tofauti kati ya misimu na lakabu ? (al. 2)
4. I) Miviga ni nini ? (al. 2)
   ii) Fafanua hasara zozote tano za miviga (al. 5)
5. I) Tambua kipera cha maka yafuatayo (al. 2)
   “ Wewe ni mbumbumbu kiasi kwamba ukiona picha yako kwenye kioo unashangaa ulimwona wapi mtu huyo”.
   i) Ngomezi ni nini? (al. 1)

## MTIHANI WA 6


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

SEHEMU YA A : TAMTHILIA

Kigogo : Pauline Kea

1. LAZIMA

"Asante ya punda kweli ni mateke. Sikujua ungekuja kunihangaisha ..."

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

b) Onyesha jinsi msemewa anamwangaisha msemaji. (alama 2)

c) Kwa kurejelea tamthilia nzima onyesha ukweli wa methali "Asante ya punda ni mateke." (alama 14)

SEHEMU B : HADITHI FUPI

Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine

Jibu swali la 2 au 3

2. "... maendeleo yanadai mchango wa kila mtu, maskini na tajiri"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Taja na ueleze sifa nne za msemaji katika dondoo hili. (alama 4)

c) Mambo yepi mengine ambayo msemaji huhojiana na wenzake wanapokutana ? (alama 6)

d) Taja na ueleze maudhui matatu yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 6)

3. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya, 'Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.' Jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi. (alama 20)

4. <u>SEHEMU YA C : USHAIRI</u>

*Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali.*

Mungu naomba subira, subira nayo imani
Imani iliyo bora, bora hapa duniani
Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani
Hiani pamwe ukora wenye kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na ufidhulu
Ufidhuli wa kudhuri, kudhuri wangu muwili
Muwili hata kidari, kidari kuwa thakili
Thakili kisinawiri, kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele
Muwele wa hitilafu, hitilafi ya nduwele
Nduwele kutakilifu, kutakilifu milele
Milele kutoniafu, kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vitomele vikwato
Vikwato pia maole, maole kufanya mito
Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto
Kitoto kilo vipele, vipele vyenye fiakuto.



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Fukuto lanipa neno, neno hili kutamka
Kutamka wazi vino, vino subira kutaka
Kutaka imani mno, mno n'sipate wahaka
Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.

Mashaka haya ya leo, leo yawe yarnepita
Yaniepita na vilio, vilia vipishe nyota
Nyota njema ingarao, ing'arao kunikita
Kunikita salamani, salamani nikadata.

*a)* Kwa nini nafsi neni inaomba subira na amani ? (alama 2)
*b)* Shairi hili ni la aina gani kwa kuzingatia : (alama 4) i) Mpangilio wa maneno ii) Mpangilio wa vina
*c)* Kwa kutokea mifano eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (alama 4)

*d)* Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)
*e)* Kwa kutolea mifano, eleza jinzi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa kutekeleza arudhi. (alama 6)

SEHEMU D: RIWAYA: CHOZI LA HERI

5. Fafanua ufaafu wa anwani chozi la heri,toa hoja zozote kumi (alama 20)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

6. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Ndimi Kisoi, dume la ukoo mtukufu
Ulojipambanua kwa mabingwa
Wachezaji hodari wa ngoma
Ndimi dume liloingia nyanjani
Makoo yakatetemeka
Yakang'ang'ania gozi kusakata nami

a) Tambulisha kipera kinachojitokeza katika kifungu hiki. (alama 2)
b) Eleza sifa tano bainifu za kipera hiki katika fasihi simulizi. (alama 10)
c) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. (alama 8)

SEHEMU F: FASIHI SIMULIZI (ALAMA 20)

7. a) Taja na ueleze vipera vya maghani. (alama 10)
b) Eleza maana ya miviga. (alama 2)
c) Fafanua sifa nne za miviga katika jamii. (alama 8)

## MTIHANI WA 7

FASIHI SIMULIZI


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

(a) Eleza maana ya tanzu zifuatazo za fasihi simulizi

(i) Ngomezi

(ii) Miviga

(iii) Wawe

(iv) Ngano za mtaanziko (al.8)

(b) Eleza sifa bainifu za maigizo (al.6)

(c) Nini dhima ya fasihi simulizi katika jamii (al.6)

RIWAYA: CHOZI LA HERI

*"Mwanangu, usimpake tope baba yako. Amekulea kwa miaka yote hii kama mwanawe, japo kwa kweli hakuzaa wewe."*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Kwa kurejelea wahusika wengine wanne wa kike katika riwaya, thibitisha matatizo manne yaliyowakumba katika jamii ya Chozi la Heri. (alama 4)

TAMTHILIA: KIGOGO

*"Tuacheni kufumbata maji kama jiwe. Sagamoyo inahitaji mabadiliko, damu nyepesi ili kuufungua ukurasa mpya*.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Zifafanue jazanda kwenye dondoo. (alama 6)

(ch) Onesha umuhimu wa msemaji katika tamthilia. (alama 10)

5. Eleza umuhimu wa wahusika wafuatao katika kuendeleza maudhui ya tamthilia ya Kigogo.

(a) Majoka

(b) Tunu

(ch) Babu (alama 20)

HADITHI FUPI: TUMBO LISI/OSHIBA NA HADITHI NYINGINE

"Mame Bakari" (Mohamed Khelef Ghassany)

*"Dunia we' dunia. Dunia ya mwenye nguvu, si ya mimi dhaifu wa nguvu. Dunia ya msumari moto juu ya donda bichi."*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
(b) Ni mbinu ipi iliyotumika katika dondoo hili? (alama 2)

(ch) Taja baadhi ya maamuzi ya maana yaliyofanywa na msemaji wa dondoo. (alama 6)

(d) Eleza matukio muhimu tangu mhusika apitie katika hali iliyo kwenye dondoo. (alama 8)

**Huku ukirejelea hadithi Tumbo Lisiloshiba, Mapenzi ya Kifaurongo na Mkubwa, fafanua madhara ya ubinafsi na tamaa. (alama 20)**

SEHEMU E. USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

yanayofuata 1. Natunga nikiwaasa, msije
kujijutia, Mitego sije wanasa, mkaja
kuangamia
Tamaa nyingi za pesa, gereza, zitawatia
Kila mpenda rushwa, jela inamkonyeza

2. Jela inamkonyeza, kama hutajizuwia Haina ndugu gereza, jela si ya kuchezea,
Inajuvya na kupoza, wenye nguvu kutulia
Kila mpenda rushwa, jela inamkonyeza

3. Rushwa si kitu chema, walaji jihadharini, Mkila zitawakwama, zitawatoka puwani,
Wazilao hulalama, si mimi ila Fulani
Kila mpenda rushwa, jela inamkonyeza

4. Ridhika na upatacho, kama moja au mbili,
Usitaraji mkocho, upatao, bwana Ali,
Tama zako za macho, zitakulea mbuli
Kila mpenda rushwa, jela inamkonyeza

5. Ni mema kemukemu, wenye vyeo kutumia
Maleba wakiwahimu, rushwa kuwaletea,
Muogopeni karimu, leba haombwi rushwa,



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Kila mpenda rushwa, jela inamkonyeza

6. Kuna wengi mahakimu, haki wanazopinduwa,
Yatima huwa dhulumu, kwa kupapia rushwa
Kwa kutaka darahimu, aso haki anapewa
Kila mpenda rushwa, jela inamkonyeza

Maswali

(a) Andika kichwa mwafaka cha shairi hili . (al.1)
(b) Taja madhara manne ya rushwa. (al.4)
(c) Eleza umbo la shairi hili. (al.4)
(d) Andika ubeti wanne katika lugha nathari. (al4)
(e) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia uhuru wake katika shairi hili. (al.3)
(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili .(al.4)
   (i) Gereza
   (ii) Mkocho
   (iii) Karimu
   (iv) Darahimu

## MTIHANI WA 8

RIWAYA: ASSUMPTA K MATEI

1) Athari ya vita katika nchi ya Wafidhina ni kioo cha bara la Afrika. Jadili (ala 20)

SEHEMU B : TAMTHILIA

Tibu swali la 2 au 3

**2.** Tusiwaruhusu watu wachache waliojazwa kasumba….kuturejesha ….hatuwezi kukubali kutawaliwa kidhalimu tena.

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b. Kwa kumrejelea mzungumzaji wa maneno haya, bainisha unafiki katika kauli hii. (alama 16) 3. Eleza jinsi mbinu ya taharuki ilivyotumika kufanikisha maudhui katika tamthilia ya kigogo. (ala 20)

SEHEMU C : HADITHI FUPI

Jibu swali la 4 au 5.

Eunice Kimaliro : Mtihani wa Maisha. 4.

"…..ilmuradi mawazo yanamwadhibu sasa"

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b. Fafanua sifa za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 6)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

c. Onyesha mawazo yanayomwadhibu anayerejelewa na dondoo hili. (alama 10 **Alfa Chokocho : Tulipokutana tena**

5. a. " Mamangu siku ile aliniamsha mapema."

i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4) ii) Tathmini umuhimu wa usimulizi wa mzungumzaji katika kuendeleza dhamira ya hadithi hii.
(a 8)

b. Onyesha jinsi mashaka linavyomwafiki mhusika mwenyewe katika hadithi ya "Ndoto ya Mashaka" (alama 8)

## SEHEMU D : FASIHI SIMULIZI

6. a. Huku ukitoa hoja sita linganisha aina mbili kuu za fasihi.(alama 6)
b. Jadili vipengele sita vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. (alama 6)
c. Jadili sifa mbili za vitanza ndimi kwa kurejelea sauti. (alama 2)
d.Tambua istuiatu zinzotokana na maelezo haya.
i. Msimulizi wa fasihi simulizi anaitwaje kwa jumla? (alama 1)
ii. Shujaa katika mighani pia anaweza kuitwa nani? (alama 1)
iii. Sherehe za kitamaduni ambazo hufungwa na jamii katika kipindi fulani maalum huitwaje?(alama 1) iv. Mavazi au vifaa vinavyotumiwa na wasanii kuakisi hali halisi ya mambo wakati wa kuwasilisha fasihi huitwaje? (alama 1)
v. Mtambaji wa hadithi hutumia ujuzi gani anapoibadilisha hadithi yake moja kwa moja mbele ya hadhira bila kuathiri usimulizi wake? (alama 1)
vi. Wanaosimuliwa ili kuonyesha kazi ya fasihi simulizi hupewa jina hili (alama 1) 7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Wakati tunywapo chai hapa upenuni,
Na kuwatazama watoto wetu
Wakicheza bembea kwa furaha.
Tujue kamba ya bembea yetu imeshalika
Na bado kidogo tutaporomoka

2. Kulikuwa na wakati ulinisukuma juu
Nikaenda zaidi ya nusu duara
Kulikuwa na wakati nilikudaka
Ulipokaribia kuanguka
Na kulikuwa na wakati tulibebana kwa zamu
Mmoja wima akisukuma mwingine amekaa

3. Wakati huo, japo tulipaa mbele na nyuma
Tulicheka kwa matumaini yaliyotiwa chumvi
Na kisha tukaongozana jikoni kupika chajio
Ilikuwa adhuhuri yetu
4. Sasa tukisubiri ndoto tusizoweza kuzitekeleza tena
Tumalizie machicha ya chai yetu ya
jioni Bila ya kutematema na kwa tabasamu
Na baada ya hapo tujilambe utamu utamu.


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Uliobakia kwenye midomo yetu

5. Tukikumbuka siku ilee ya kwanza
Tulipokutana jioni chini ya mwembe
Tukitafuta tawi zuri gumu
La kufunga bembea yetu
Naye mbwa simba akisubiri

6. Lakini kabla hatujaondoka kimya kimya
Kukamilisha nusu duara iliyobaki
Tuhakikishe vikombe vyetu ni safi. (E. Kezilahabi)

MASWALI

a. Fafanua maana ya kijuujuu na maana ya kitamathali ya shairi hili. (alama 4)
b. Bainisha matumizi ya vipengele vifuatavyo katika shairi. (alama 6)
i. Usimulizi. ii. Usambamba. iii. Taswira
c. Tambulisha mzungumzaji (nafsi neni) katika shairi hili. (alama 2)
d. Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)
e. Eleza maana ya mshororo " Tuhakikishe vikombe vyetu ni safi." (alama 2)
f. Changanua muundo wa shairi hili. (alama 4)

8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Tuunganeni vijana, ili tugawane kazi,
Wazee nguvu hatuna, mazito hatuyawezi,
Bora kubadilisha, nanyi vichanga vizazi.

Sisi tulijulikana, miaka iliyopita,
Tulipokuwa vijana, wenye siha na mafuta.
Vikali tulipambana, kuguru mawanda ya vita.

Tulipigana kiume, kuwang'oa walowezi,
Mikuki yetu na sime, ilichimba yao mizizi
Ikawabidi wahame, kugura yetu makazi.

Ni kazi itambueni, tuliyoyafanya wahenga,
Nchi tumeiauni, tokana na kubwa janga, Sasa
vijana linden, na wazee twaijenga.

Mjitolee maisha, kuilinda kwa adabu.
Muize kuibadilisha, japo mupewe dhahabu,
Wazee tutawalisha, kama ilivyo wajibu.

Toka pwani hadi bara, vijana nchi linden



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724251706)

Tokeni muwe imara, hasa humo mipakani,
Ajaribuye kupora, vijana mchafueni.

Onyesheni uzalendo, washtuke vibaraka
Muonyeshe kwa vitendo, na nia zilosafika
Mujivue na mwenendo,tamaa ya madaraka

Twawahusia wazee, wakongwe wenye ujuzi,
Kabisa msilegee, kuridhia upuzi Mtu
asiwachezee, katika yetu makazi.

MASWALI

a. Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili.
b. Bainisha nafsi neni na nafsi nenewa katika shairi hili.
c. Eleza bahari zozote tatu kwa shairi hili.
d. Andik ubeti wa tatu kwa lugha nathari.
e. Huku ukitoa mifano, onyesha aina mbili za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili.
f. Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na namna yaliyotumika katika shairi.
 i. Walowezi ii. Tumeiauni.
g. Pendekeza anwani mwafaka katika shairi hili.

## MTIHANI WA 9

USHAIRI

*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Ewe baba mwenye kipara, huna aibu kuniita?
Kwa kuwa unayo mipesa, wautumia wangu mwili
Watumieni huu mwili, kama chombo kujiliwaza
Waniweka kwa lako gari, hata yake bei sijui
Acheni wako uhuni.

Bado miaka sijatimu, wewe mama wanionyesheni
Wanipeni nifanye kazi, kazi hizi huwa ni nyingi
Wakati mwingine hunilipi, eti nami nina faida
Sikitaki chakula hiki, kina uchungu ndaniye
Acheni wako uhuni.

Nguo nzuri wanunua, waniita eti supuu



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851706)

Nami nikuite dadii, tuweze kushikana kote
Nami kwa kuwa nahitaji, yabidi nikutegemee
Nimekubali unicheze, sawa mpira uwanjani
Acheni wako uhuni.

Mizigo mizito nabeba, ukiniiteni shamba boi
Nikosapo wanichapeni, kisahau wakosa pia
Lakini usiku 'kifika, mimi si shamba boi tena
Nikutoe wako uchovu, kupapasa wako mgongo
Acheni wako uhuni.

Kwa kuwa unazo mihela, wambembeleni babangu
Unampeni zako pesa, ili niwe ni lako chungwa
Bado miaka sijatimu, lakini kwako nimeiva
'kiniona mate hukutoka, eti "umeiva ka' nyanya"
Acheni wako uhuni.

Nimefanyeni maajabu, hata mbele ya maulana
Kulaleni nawe mzee, ukisema mimi ni poa
Na kwa wangu ujinga pia, 'meangukia ukarimu
Lakini wako ukarimu,Umeanzeni kinighasi
Acheni wako uhuni

**Maswali**

a) Andika kichwa mwafaka cha shairi hill. (Alama l)
b) Tambua idhini **moja** ya kishairi katika shairi na uifafanue (Alama 2)
c) Ainisha shairi hill kwa bahari **mbili** tofauti (Alama 4)
d) Eleza **umbo** la shairi hili (Alama 4)
e) Tambua wahusika katika ubeti wa **pili** (Alama 2)
f) Andika ubeti wa mwisho katika **lugha nathari**. (Alama 4)
g) Bainisha maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi. (Alama 1)
   i) Kunighasi
h) Eleza swala **moja** linalojitokeza katika ubeti wa **tano** (alama 2)

TAMTHILIA: KIGOGO

*"Nilijua huwezi kuniacha katika hali hii ya tuhuma.*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua sifa za msemaji wa dondoo. (alama 16)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

RIWAYA: CHOZI LA HERI

*"Haiwezekani! Hili haliwezekani! Itakuwa kama kile kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike; yule anayesimuliwa katika visakale vya majirani zetu."*

(a) Eleza mkutadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Onesha jinsi wahusika wa kike katika riwaya walivyojitahidi kuleta mabadiliko yenye manufaa katika nchi ya Wahafidhina. (alama 16)

*"Ni kweli watu wana haki ya kusamehewa, kwani hakuna binadamu hata mmoja aliyekamilika." Kwa kurejelea riwaya, jadili kauli hii.* (alama 20)

HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE:

"Tulipokutana Tena" (Alifa Chokocho)

*"Hivi ndivyo maisha yapasavyo kuwa-huru kabisa."*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Ukirejelea hadithi, thibitisha kuwa mmoja wa wahusika hawa hakuishi maisha ya awali inavyopasa. (alama 16)

*Fafanua maudhui ya umaskini yanavyojitokeza katika hadithi Tumbo Lisiloshiba na Tulipokutana Tena. Zingatia hoja nne nne kwa kila hadithi.* (alama 20)

FASIHI SIMULIZI

a) i) Tambua njia **tatu** za kuhifadhi kazi ya fasihi simulizi (alama 3) ii) Taja matatizo yanayoweza kumkabili mkusanyaji wa kazi za fasihi simulizi. (alama 4)

(b) Tambua majukumu matatu ya **lakabu** (alama 3) (c) i) Eleza maana ya **misimu** (alama 1) ii) Fafanua jinsi ambavyo **misimu** hutokea (alama 4) iii) Dokeza majukumu **matano** ya **misimu** (alama 5)

MTIHANI WA 10

SEHEMU A: RIWAYA.
Assumta k matei
1.Jadili Dhana ya chozi katika riwaya ya Chozi la Heri (alama 20)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

SEHEMU B: TAMTHILIA

**Pauline Kea:** Kigogo

**Jibu swali la 2 au la 3.**

2. " Do ! Do ! Simameni ! Simameni leo kutanyesha mawe! "
   i) Eleza muktadha wa dondoo hili. ( alama 4)
   ii) Fafanua mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo (alama 4) iv) Dhihirisha kwa kuzingatia hoja sita jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika tamthilia ya " Kigogo." (alama 12)

**au**

3) Eleza kwa kutolea mifano mitano mitano jinsi mwandishi alivyofaulu kutumia mbinu za :
i) majazi (alama 10)
ii) mbinu rejeshi (alama10)

SEHEMU C: HADITHI FUPI

**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda:**

**Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine**

**Jibu swali la 4 au la 5.**

4. i) Sekta ya elimu ina changamoto nyingi.Thibitisha kwa kurejelea hadithi zifuatazo(alama 20) a) Mapenzi ya Kifaurongo
b) Shogake dada ana Ndevu
c) Mwalimu Mstaafu
d) Mtihani wa maisha

**au**

5) '' Hakikubakia hata chakula kidogo cha sadaka ya mwenye njaa… ''
   i) Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja kumi ukirejelea hadithi ya Tumbo Lisiloshiba(al 10) ii) Jadili uhalisia wa hadithi ya Tumbo Lisiloshiba katika jamii ya leo kwa kutoa hoja kumi.(al 10)

SEHEMU D: USHAIRI

**Jibu swali la 6 au la 7.**

*6. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Dunia kitu dhaifu, si ya mtu kunyetea,
Usione ufanifu, na furaha kila njia,
Kumbuka na uvunjifu, kama ndwele hukujia,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

Anasa usiandame, kwa pupa kuzipapia,
Heri moyo fanye tume, uche na kuzikimbia,
Hakuna mume wa dume, na wala hatatokea,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

Wako wapi mashujaa, wenye nguvu kila njia,
Ziliwafika nazaa, wakabaki kujutia,



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Ndunia ina hadaa, yataka kuzingatia,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu
silewelewe.

Kam kam mahuluki, viumbe vyake jalia,
Walokuwa na maluki, bora za kujivunia,
Muda wakitahamaki, iliwatupa dunia,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu
silewelewe.

Fikiri zao sharafu, walizo wakitumia,
Penye unasi alifu, wanenalo maridhia,
Mwisho wayo madhaifu, na majina
kupotea, Tagaa bovu dunia, ndu yangu
silewelewe.

Walishushwa ghorofani, mapambo na mazulia,
Wakawachia wandani, na mali zilizosalia,
Wameshia kaburini, udongo kuwafukia,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

Naturudi kwa manani, tutubu zetu hatia,
Kwa baraka za Amini, Mola tatughofiria,
Tutafuzu duniani, mema na ahera pia,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu
silewelewe.

Turudipo kwa Jalali, tukayawacha mabaya,
Kila sada tutanali, na shari kutwepushiya,
Tutapata na uvuli, ahera kujifichiya,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

<u>MASWALI :</u>

a) Fafanua ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa nne. (alama 3)

b) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 3)
   (i) Idadi ya vipande katika mishororo
   (ii) Mpangilio wa vina katika mishororo
   (iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti

c) Taja na ueleze tamathali mbili za kifasihi zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)

d) Andika aina tatu za uhuru wa kishairi zilizotumika katika shairi hili. (alama 3)

e) Andika ubeti wa sita katika lugha tutumbi. (alama 4)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724251796)

f) Bainisha toni ya shairi hili. (alama 1)

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. i. Kunyetea ii. mahuluki (al 2)

*au*

*1.Soma shairi hili kisha uyajibu maswali yafuatayo:*

Ni sumu, sumu hatari
Unahatarisha watoto
Kwa ndoto zako zako leweshi
Za kupanda ngazi
Ndoto motomoto ambazo
Zimejenga ukuta
Baina ya watoto
Na maneno laini
Ya ulimi wa wazazi

Ni sumu, sumu hasiri
Unahasiri watoto
Kwa pupa yako hangaishi
Ya kuwa tajiri mtajika
Pupa pumbazi ambayo
Imezaa jangwa bahili
Badala ya chemichemi
Ya mazungumzo na maadili
Baina ya watoto na mzazi

Ni sumu, sumu legezi
Unalegeza watoto
Kwa mazoea yako tenganishi
Ya daima kunywa 'moja baridi'
Mazoea mabaya ambayo yanafunga katika klabu
Hadi saa nane usiku
Huku yakijenga kutofahamiana
Baina ya watoto na mzazi

Ni sumu, sumu jeuri
Unajeruhi watoto kwa pesa,
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye madawa ya giza baridi
Barabara inayofikisha kwenye giza baridi la kaburi la asubuhi



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

MASWALI :

a) Andika mifano miwili ya mistari mishata katika shairi hili. (alama 2)
b) Fafanua maudhui yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 4)
c) Fafanua umuhimu wa urudiaji katika shairi hili. (alama 4)
d) Bainisha nafsi neni na nafsi nenewa katika shairi hili. (alama 2)
e) Yanayozungumziwa yanajenga ukuta kwa njia gani. (alama 4)
f) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari. (alama 4)

8. SEHEMU E :FASIHI SIMULIZI

(a) Eleza sifa tano za miviga. ( alama 5)

(b) Huku ukitoa mifano, onyesha udhaifu wa miviga. (alama 5)
(c ) Taja aina za miviga ambayo hupatikana katika jamii ya kisasa.. (alama 5)
(d ) Eleza nafasi ya miviga katika jamii.

MTIHANI WA 11

USHAIRI

1. Shairi la E. M Nbuthia

Jiji
Lilojaa fahari na vinyume.

Maghorofa
Yatishayo kupasua ngozi ya
mawingu Viumbe na magari
Waliobanana barabarani.

Jiji la
Waliostaarabika
Ya kidunia,
Mafukara.

Lililojaa mfaano na mwambatano.
Wa majalala ya taka na waokotezaji
Wa ombaomba na waliotakata
Wa polisi na dereva
Wa waliopujuka na wanaostahi

Jiji la:



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Majengo ya aushi na mioyo ya mawe
Jua linalooka viumbe
Jua linalotekenya ngozi za watalii – wakimbiao ganzi ya majibaridi          Jua lichomao wavuja jasho          Huku wakizumbua riziki.

La viwanda
Vijazao vibeti vyenye mamba vya wenye viwanda
Vinavyofuka moshi kwenye madongoporomoka
Vinavyosumu maisha machanga na kuua wasiozaliwa.

Jiji
La wazururao na manamba
Wanaotia kitanzi staha
Wanaotoa kauli na maneno
Yanayouma na kukereketa
La wazee na vijana
Ambao taadhima yao
Imemezwa na jiji juani.

Jiji litandalo mashariki na magharibi
Kaskazini na kuini
Mbuga zitandao
Katikati ya tanuru hili
Litengalo sehemu kwa baadhi
Majumba vilimani
Vyumba visivyo dari
Na mabanda yaso dirisha
Kusugua mikono laini ya mwenye nyumba.

(a) Fafanua kilichompa mtunzi wa shairi hili msukumo wa kulitunga. (alama 4)
(b) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
(c) Taswira zinazojengwa katika ubeti wa 6 zina umuhimu gani? (alama 6)
(d) Jua linaelekea kupewa umbele katika shairi hili kwa nini? (alama 2)
(e) Taja na utolee mifano aina mbili za uhuru wa mtunzi zinavyojitokeza tungoni. (alama 2)
(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)
    (i) Waliotakata.
    (ii) Wanatia kitanzi staha,



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

TAMTHILIA: KIGOGO

Jadili matumizi ya majazi katika tamthilia ya Kigogo huku ukitoa mifano miwili kwa kila jina. (Alama 20)

RIWAYA: CHOZI LA HERI

*"Mtu anayekusikiliza atadhani kwamba umekulia katika mazingira sawa na Sisi wanyonge ambao uwepo wetu unaamuliwa na matajiri."*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

(b) Fafanua tamathali ya usemi iliyotumika na msemaji wa kauli hii.. (Alama 4)

(ch) Fafanua sifa za mrejelewa katika kauli hii. (Alama 12)

*"Wakati wa mabadiliko umefika. Wimbi la mabadiliko limevamia jamii yetu." Jadili mabadiliko yaliyotokea na athari zake katika nchi ya Wahafidhina. (Alama 20)*

HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA ILADITHI NYINGINE:

"Mtihani wa Maisha" (Eunice Kimaliro)

“ilmuradi mawazo yanamwadhibu sasa. “

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua sifa sita za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 6)

(ch) Taja mambo mbalimbali yanayochangia adhabu ya mrejelewa wa dondoo hili. (alama 10)
5. Kwa kurejelea hadithi zozote tatu katika Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine, onesha vile waandishi walivyotumia mbinu ya taswira. (alama 20)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) (i) Eleza maana ya miviga. (alama 2)
(ii) Taja aina zozote **tatu** za miviga. (alama 3)
(iii) Eleza hasara zozote **tano** zinazohusishwa na miviga. (alama 5)
(b) Fafanua sifa zozote **tano** za ulumbi. (alama 10)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

## MTIHANI 12

SEHEMU YA A – RIWAYA: *CHOZI LA HERI*

1. Huku ukitolea hoja zozote kumi riwayani, fafanua nafasi ya mwanamke katika jamii (alama 20)

SEHEMU YA B – TAMTHILIA: *KIGOGO*

**Jibu swali la 2 au 3**

2. "Dalili ya mvua ni mawingu, lazima tuwe macho".

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)

(c) Ushauri uliotolewa na msemaji baadaye kama njia mojawapo ya kuwa macho ni wa kidhalimu. Fafanua. (alama 4)

(d) Eleza namna unafiki wa msemaji na upumbavu wa mnenewa unavyodhihirika katika muktadha wa dondoo hili.(alama

(e) Onesha jinsi ukweli wa kauli hii ulivyojitokeza baadaye katika tamthilia. (alama 4)

3. Jadili migogoro inayojitokeza katika tamthilia ya *kigogo*, kisha utathmini namna ilivyosuluhishwa. (alama 20)

SEHEMU YA C:HADITHI FUPI: *TUMBO LISILOSHIBA*

**Jibu swali la 4 au 5** 4. "Kesho kama sote tutaamka salama……….kama tutafungua milango ya nyumba zetu"….

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4) (c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)

(d) Hadithi hii inaakisi mambo mengi yanayotendeka katika bara la Afrika. Taja mambo sita (alama 6)

5. Ukengeushi huzorotesha maendeleo ya kijamii. Jadili kauli hii ukirejelea hadithi ya 'Mkubwa'. (alama 20)

SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI

6. (a) Eleza vipengele vitano vya fasihi simulizi ambavyo hujitokeza katika fasihi andishi.(alama 10)

(b ) Fafanua sifa tano za ushairi simulizi. (alama 10)

SEHEMU E: USHAIRI

**7. Soma mashairi haya kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Shairi A

Umekata mti mtima
Umeangukia nyumba yako
Umeziba mto hasira
Nyumba yako sasa
mafurikoni Na utahama
Watoto kuwakimbia.

Mbuzi kumkaribia chui
Alijigeuza panya
Akalia kuliwa na paka kichwani



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Mchawi kutaka sana
kutisha Alijigeuza samba
Akalia na risasi kichwani.

Jongoo kutaka sana kukimbia
Aliomba miguu elfu
Akaachwa na nyoka

Hadija wapi sasa utakwenda
Bwanako kumpa sumu? Hadija
umemshika nyoka kwa mkia,
Hadija umepita nyama ya Punda.

Shairi B

Piteni jamani, Piteni haraka
Nendeni, nendeni huko mwendako
Mimi haraka, haraka sina,
Mzigo wangu, mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuweka.

Vijana kwa nini hampiti?
Kwa nini mwanicheka kisogo?
Mzigo nilioubeba haupo kichwani
Lakini umenipinda mgongo na
miguu Na lazima nijiegemeze,
kichwani Chini nendeko.

Haya Piteni! Piteni! Haraka! Heei!
Mwafikiri mwaniacha nyuma!
Njia ya maisha ni moja tu
Huko mwendako ndiko nilikotoka
Na nilipofikia wengine wenu
Hawatafika.

Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati
Lakini kama mnepita mbele
Na uso wangu kuutazama Ningewambia siri ya miaka mingi.

<u>MASWALI</u>

(a) Haya ni mashairi ya aina gani? (al.1)
(b) Washairi hawa wawili wanalalamika. **Yafafanue** malalamishi yao. (al.4)
(c) Onesha vile kinaya kinavyojitokeza katika tungo hizi mbili. (al.6)
(d) Kwa kurejelea shairi 'B'**eleza** maana ya: (al.3)
  (a) mzigo


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351796)

(b)Siri

(c) Niko nyuma ya wakati

(e) **Andika** ubeti wa kwanza wa shairi 'A' kwa lugha nathari (alama 4)

(f) Uhuru wa mshairi umetumiwa vipi katika shairi 'B' (alama 2)

## MTIHANI 13

USHAIRI

Linatushangaza, twashangaa dhidi ya kushangaa!
Kwa mangamizi ya kila leo.
Tunayotekelezewa na kiumbe razini zaidi,
Binadamu!

Hatujui sababu,
Mzinga na mazega yetu kuteketezwa,
Yetu asili kuvinwa kwa mababu na waritimba,
Binadamu wasiojua madhila yetu
Kudamka kutafuta nekta, na kukesha kulinda mzinga!
Lakini kinachotushangaza, twauliza: mwatuchomeani?

Twafedheka jamani!
Masaibu ya tajiri
Tajiri mwema kuwatajirisha wasio na faidha
Badala ya wakatilia moto daraja la fanaka,
Wasijue kesho, kesho kutwa, mtondo…. Watavuna wapi?
Baada ya kutuangamiza, sie vitega chumi vyao.

Tuma haki, kama nyinyi,
Ya kuwaona watoto na wetu vijukuu
Wakikua na kufaidi, jasho letu wazazio
Ingawa hili halijawa faradhi,
Ila kwa mapenzi yenu ya dhati


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Kumbuka binadamu,
Hata sisi tuna hisia, tusichomwe,
Japo wajinga tunayo manufaa
Sie hatuwahi, mbona nyie?
Na safari yetu sote, japo njia tofauti.
Twende pole pole!

Maswali

a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (ala. 2)

b) Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu. (ala.4)

c) Taja na utoe mifano miwili ya tamathali za semi zilizotumiwa katika shairi hili. (ala. 4)

d) Huku ukitoa mifano mwafaka eleza idhini za utunzi zinazojitokeza katika tungo. (ala. 4)

e) Eleza maana ya msamiati ufuatao:

i) Razini ii)

Masaibu

f) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (ala. 4)

HADITHI FUPI: "NIZIKENI PAPA HAPA" (Ken Walibora)

*"Kauli yake ni kama maji ya moto yasiyoweza kuchoma nyumba."*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

(b) Taja na ueleze umuhimu wa tamathali moja ya usemi iliyotumika katika dondoo. (Alama 2)

(ch) Fafanua sifa za wapuuzaji wa kauli iliyotolewa. (Alama 8)

(d) Jadili dhima sita za mrejelewa katika dondoo. (Alama 6)

TAMTHILIA: KIGOGO

*"Nako kuelimika Sio kustaarabika. Hebu jiangalie, heri mimi wa kisomo cha msingi."*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

(b) Taja mambo matatu ambayo msemaji anamwambia msemewa katika onyesho hili. (Alama 3)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851786)

(ch) Jadili sifa za msemaji wa kauli. (Alama 13)

*Jadili matumizi ya jazanda katika tamthilia ya Kigogo. (Alama 20)*

RIWAYA: CHOZI LA HERI

*Ndio. Sijui kwa nini watu hawa hawajifunzi kutokana na majanga yanayowakumba wenzao...*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

(b) Onesha changamoto zilizomkabili msemaji na wenzake katika kuwashughulikia wanaolengwa katika siku za awali. (Alama 6)

(ch) Fafanua majanga kumi yanayowakabili watu wa rika la warejelewa katika dondoo. (Alama 10)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

2. a) Eleza tofauti kati ya maghani na mighani. (ala.2)

b) Eleza jinsi utakavyowasilisha utanzu wowote wa fasihi simulizi. (ala. 8)

c) Je, ni vipi jamii ya kisasa inaendeleza fasihi simulizi. (ala. 6)

d) Eleza mambo manne ambayo huchangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (ala. 4)

## MTIHANI 14

RIWAYA: CHOZI LA HERI

*"Ni kweli binti yangu, kwa kutumia falsafa hii, una haki ya kusema Sisi tu watoto wa miaka hamsini."*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Eleza maana ya kauli: 'tu watoto wa miaka hamsini' kwa mujibu wa dondoo. (alama 2) (ch)

Tetea ukweli wa kauli hii kwa kurejelea matukio katika riwaya. (alama 14)

TAMTHILIA: KIGOGO

*"Si maandamano ya wauguzi yalisitishwa jana ... Walimu wamegoma tena wakiwa likizoni?"*

(a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)

(b) Eleza sababu za maandamano na migomo kwenye tamthilia. (alama 8)

(ch) Fafanua sifa tatu za msemaji wa maneno haya. (alama 8)

*Jadili jinsi mwandishi wa Kigogo alivyofaulu katika kutumia mbinu*

*zifuatazo:* a) Sadfa

b) Takriri

c) (b) Kisengere nyuma

d) Jazanda

e) Kinaya (alama 20)

HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE "Shibe Inatumaliza" (Salma Omar Hamad)

"Ubadhirifu unaotendeka katika jamii unatokana na uzembe na mapuuza ya wanajamii. Onesha ufaafu wa kauli hii kwa kurejelea hadithi: Shibe Inatumaliza.

SEHEMU YA D-USHAIRI

6. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

1. Ni sumu,sumu hatari
Unahatarisha watoto
Kwa ndoto zako leweshi
Za kupanda ngazi,
Ndoto motomoto ambazo
Zimejenga ukuta
Baina ya watoto
Na maeneo laini
Ya ulimi wa wazazi

2. Ni sumu ,sumu hasiri
Unahasiri watoto
Kwa pupa yako hangaishi
Ya kuwa tajiri mtajika,
Pupa pumbazi ambayo
Imezaa jangwa bahili
Badala ya chemichemi
Ya mazungumzo na maadili
Baina ya watoto na mzazi

3. Ni sumu ,sumu legezi
Unalegeza watoto
Kwa mazoea yako tenganishi
Ya daima kunywa 'moja baridi'
Mazoea mabaya ambayo
**Yanakufunga katika klabu**
Hadi saa nane usiku
Huku yakijenga kutofahamiana
Baina ya watoto na mzazi

4. Ni sumu ,sumu jeruhi
Unajeruhi watoto kwa pesa
Kuwa mapenzi yako hatari
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye madawa ya kulevya
Barabara inayowafikisha kwenye **giza baridi**
La kaburi la asubuhi

**(kutoka :Bara jingine,K.Wa Mberia Marimba ,uk 48-49)**

(a) Pendekeza kichwa kwa shairi hili.
(alama



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

1)

(b) Fafanua maudhui ya shairi hili. (alama 4)

(c) Ni kwa njia gani kinachozungumziwa kinajenga ukuta? (alama 2)

(d) Dondoa tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi na uzieleze . (alama 4)

(e) Eleza umbo la shairi hili (alama 3) (f) Uandike ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 4)

(g) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi:

(i) Giza baridi

(ii) Yanakufunga katika klabu (alama 2)

FASIHI SIMULIZI

(a) Huku ukirejelea jamii yoyote ya Kiafrika ,andika miktadha ambamo ushairi simulizi ulijikita (alama10)

(b) Maigizo huchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi.Thibitisha (alama10)

## MTIHANI WA 15

SEHEMU A:USHAIRI

Jinalo limetukuka, kutoka jadi mwanzoni
Milele hutadunika, hata kwa pigo vitani
Ulugha uloumbika, muundo wa wasitani
Hakuna wa kukuponda; mwana mwema Kiswahili

Kila anokuutamka, hukunyambua kifani
Hasemi kuhakahaka, ja mwana wa uchangani
Vitabuni kitumika, hupumbaza nyoyo ndani
Na milele hutavunda, mwana mwema Kiswahili

Mja akikitamka, mwenyeji ama mgeni
Msikizi huridhika, ungiavyo mdomoni
Humwondokea wahaka, ukapenya sikioni
Hapana wa kukushinda, mwana mwema Kiswahili

Vitabuni huchipuka, ukashawishi maoni
Hutuwili kila rika, wakatukuza nishani
Nami ninakuzindika, usambae duniani
Hawapi wa kukukinda, mwana mwema Kiswahili

Kiswahili tokatoka, uenee duniani Kila



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

baidi we fika, pembe'ne ulimwenguni
Ukizamishwa ibuka, uabiri kila kani
Hazuki wa kukushinda, mwana mwema Kiswahili

Kwa vina umeumbika, umeshinda kilatini
Na mizani za mwafaka, utamkwapo wimboni
Nishani nitakutwika, utamalaki maoni
Hazuki wa kukushinda, mwana mwema Kiswahili

Nakuaga mtukuka, Kiswahili mwenye mboni
Kitabuni nakuweka, wasome mamilioni
Utuwe kusalimka, maombi ya mwarandani
Hayuko wa kukufyanda, mwana mwema Kiswahili

*Maswali*

1 Pendkeza anwani inayofaa shairi hili (al. 2)
2 Ni mbinu gani ya lugha ambayo Imetumika katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa pili (al. 2)
3 Eleza toni ya shairi hili (al. 2)
4 Uhuru wa kishairi umetumikaje katika shairi hili (al. 3)
5 shairi hili linaweza kuwekwa katika bahari gani. Taja mbili (al. 2)
6 Eleza muundo wa shairi (al. 4)
7 Mshairi anatoa ujumbe gani katika ubeti wa sita (al. 3)
8 Eleza maana ya: (al. 2)

- Na milele hutavunda
- Kiswahili mwenye mboni

SEHEMU B:CHOZI LA HERI

2 Jadili nafasi ya vijana katika kuleta mabadiliko katika jamii (al 10)
3 jadili umuhimu wa mashirika ya misaada ukirejelea riwaya hii (al 10)

SEHEMU C:KIGOGO

4 " Mguu huu ni wako"

- Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
- Ni tamathali gani ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. Eleza maana yake (al.2)
- Msemewa alipewa ahadi zipi (al. 5)
- Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji (al. 9)

5 Eleza mbinu ya

- Majazi (al.10)
- Kinaya (al.10)

SEHEMU D:TUMBO LISILOSHIBA

Kwa kuzingatia hadithi zozote tano eleza uozo wa jamii kama unavyojitokeza katika tumbo lisiloshiba (Diwani)

7 "Kesho panapo majaaliwa. Kesho kama sote tutaamka…….. kama tutafungua milango ya nyumba zetu zinazosimamia juu ya ardhi hii adhimu…"



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

a Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
b Eleza sifa nne za msemaji (al. 4) c)
Taja mbinu zozote mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili (al. 2) d
Kwa kurejelea hadithi nzima onyesha namna jamii ya kisasa ina tumbo lisiloshiba (al. 10)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8 a Eleza maana ya miviga (al. 2)
B Taja mifano mitano ya miviga katika jamii za kiafrika, kabla ya kuja kura wamishenari (al.5)
C Eleza majukumu ya miviga (al. 5)
D Taja na ueleze vitambulishi vya fasihi simulizi (8)

MTIHANI WA 16

FASIHI SIMULIZI

(a)Maigizo ni nini? (al.2)
(b) Taja vipera vyovyote viwili vya maigizo (al.10)
(c) Eleza dhima zozote tano za maigizo (al.10)
(d) Jadili njia zinazotumiwa na kizazi cha sasa kuendeleza utanzu huu. (al.6)

HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE "masharti ya kisasa" (alifa chokocho)

*"...nataka ujue kwamba mimi ni mwanamke wa kisasa, na mwanamke wa kisasa hutafuta mwanamume wa kisasa."*

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)

(b) Anayesema haya alikuwa na sifa zipi? (Alama 8)

(ch) Anayeambiwa maneno haya alijua maana ya usasa? Thibitisha. (Alama 8)

RIWAYA: CHOZI LA HERI

*"Nilipojaribu kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika.*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

(b) Fafanua mambo mbalimbali yaliyomfika anayesema maneno katika dondoo hili. (Alama 8)

(ch) Ridhaa aliyapitia maisha kama ya mhusika kwenye dondoo. Yataje. (Alama 8)

*"Moja ya mambo yanayijitokeza katika Chozi la Heri ni migogoro ya kinasaba." Jadili. (Alama 20)*



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724251706)

TAMTHILIA: KIGOGO

*"Na katika uchu huo huo amependa kukifikia kilele cha ufanisi kwa kukanyaga migongo ya wenziwe."*

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)

(b) T aja na uthibitishe mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (Alama 4)

(ch) Onesha mchango wa mzungumzaji katika tamthilia. (Alama 12)

*(a) Onesha jinsi mbinu ya majazi ilivyotumiwa katika tamthilia. (Alama 12)*

*(b) Nini umuhimu wa jazanda katika kuiendeleza tamthilia? (Alama 8)*

SEHEMU YA E USHAIRI

VITA VYA NDIMI

Huyo !Amshike huyo !
Hakuna bunduki wala kifami
Bomu na risasi hata hawazijui
Lakini mno wanashambuliana
Kwa ndiMi zilizonolewa kwa makali
Vipande vya matusi silaha zao

Yu imara mmoja wao
Akirusha kombora la nenO zito!
Linitingishe adui wake
Na kumgusa hisia kwa pigo kuu
Pigo linalochoma moyoni kama kichomi
Kuchipuza joto la hasira na kisasi
Katika mapigano yaso na kikomo

Filimbi ya suluhu inapulizwa kuwaamua!
Ni nai anayekubali suluhu?
Roho zinakataa katakata
Huku ukaidi ukinyemelea na kutawala kote
Mapandikizi ya watu
yakipigana Vita shadidi
visivyo ukomo Vita vya ndimi!

Magharibi sasa
Jua linapungia mkono machweo
Nalo giza likinyemelea kwa kiburi na
Kasi



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851796)

Sisikii tena sauti za mIsonyo
Mate ya watesi yamekauka
Makanwa yao yamelemewa na uchovu
Sasa wameshikana mikono
Ishara ya suluhu

*Maswali*

(a) Hili ni shairi la aina gani? (al.1)
(b) Eleza dhamira ya mshairi (al.2)
(c) Eleza siFa za utunzi alizotumia mshairi (al.3)
(d) Taja tamathali zozote tatu alizotumia mshairi (al.3)
(e) Eleza toni ya mshairi katika beti tatu za awali (al.1)
(f) Eleza hatima ya yanayozungumziwa kwenye shairi (al.1)
(g) Mshairi ametumia alama hisi kwingi. Eleza umuhimu wake (a.1)
(h) Itambue nafsi neni katika shairi (al.1)
(i) Andika mishororo ya kwanza mitatu ubeti wa 4 kwa lugha ya nathari (a.3)
(j) Toa maana ya msamiati huu (al.2)
(i) Kombora
(ii) Misonyo

Ndege mwema na muruwa, katu haishi tunduni
Hataki kufadhiliwa, muda yumo utumwani
Japo mnyonyoe mbawa, mwisho wake utahuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege ataka yoyoma, nasiyahi msituni
Apite akisimama, shinani na mitawini
Haridhiki kwa mtama, na maji ya kikombeni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa hishima mwema mno wa kughani
Tundu huliona chama, japo liwe la thamani
Huporomosha yakwe kima, na kufanya faraghani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mpambe kwa zari, na lulu na marijani
Upambe yake suduri, kwa almasi kidani
Tunduni atahajiri, ili awe huriani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Ndege mwema wa busara, hatoishi kifungoni
Anayo kubwa hasara, kukosa nyumba ya mani
Lamkera lamkera, tundu la dhahabu kwani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege maumbile yake, na waja hayalingani
Yeye hutaka wenzake wafukuzane hewani
Jambo la kuishi pweke, kamwe humridhiani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Baiti zangu ni haba, nakonea kituoni
Ndege huficha mahaba, kama yumo kifungoni
Hali ndege akashaba, kwani yumo adhabuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Maswali

(a) Lipe shairi anwani mwafaka (al.1)
(b) Fumbua maana ya ndege anayerejelewa (al.1)
(c) Shairi hili ni la mkondo gani? (al.3)
(d) Eleza muundo wa ubeti wa nne (al.3)
(e) Fafanua uhuru aliotumia mshairi (al.4)
(f) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (al.4)
(g) Jadili dhamira ya mshairi (al.2)
(h) Fafanua maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa na mshairi (al.2)
(i) Alahuni
(ii) Baiti

## MTIHANI WA 17

USHAIRI (LAZIMA)

*Soma shairi hili kasha ujibu maswali*

| | |
|---|---|
| 'Mepewa macho nione | nami sitayatumbuwa |
| Vikondefu na vinene | nipate kuvichunguwa |
| Pema na penye swenene | la kuwa na kutokuwa |
| Vipe nione mavune | nambie raha muruwa? |



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724251706)

Nimepewa macho    sitayatofowa!

'Mepewa na sikiyo katu    sitolikwanyuwa
Ya kweli na singiziyo    nipate kuyabaguwa
Vipi 'sikie kemeyo    nite sauti ya hawa?
Binadamu yake nia    tamu pate 'sikia
'Mepewa sikiyo    sitalibanduwa!

'mepewa na pua hino    kamwe sitaing'watuwa
Vioza pia vinono    puani kunukuliwa
Mnaso wake na vuno    na mnuko kuchenguwa
Vipi nisinuse pano    na kule kuna shuruwa?
Mepewa na puwa    sitaimeguwa!

'Mepewa huu ulimi    nami sitaunyotowa
Nitakalamu usemi    wenye nia na afuwa
Na maonjo vya vinyemi    sina budi kuchaguwa
Vipi nisionje kumi    na naoja nimecheuwa?
'mepewa ulimi    sitausokowa!

Nimepewa na hii ngozi    Katu sitaibanduwa
Hisia zinajalizi    zipate kusisimuwa
Nyengine za maliwazi    nyengine za kubabuwa
Vipi nisihisi twezi    ngozi ikibabuliwa?
'Mepewa na ngozi    sitoichunuwa!

Nimepewa na nadhari    kupima na kupimuwa
Nende mwendo wa kadiri    wa kuhisi na kujuwa
Wa ku'zepuka hatari    zote zinokusudiwa
Vipi mimi nihiyari    hisia zangu kutwawa?


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

‘Mepewa nadhari sitoiondowa!

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (alama 1)

(b) Shairi hili ni la bahari gani? (alama2)

(c) Eleza mtindo wa shairi hili (alama4)

(d) Eleza ni kwa nini mshairi ametumia ritifaa katika shairi hili (alama2)

(e) Eleza muundo wa shairi (alama 4)

(f) Huku ukitoa mifano eleza vile mshairi alivyotumia uhuru wa kishairi (alama2)

(g) Taja ‘hisi’nne zilizotajwa na mshairi. (alama 2)

(h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi. (alama 3)

(i) Swenene

(ii) vioza

(iii) Twezi

TAMTHILIA KIGOGO

a) Eleza jinsi Majoka anavyosaidia kuendeleza maana ya tamthilia ya Kigogo. (alama 5)

b) Eleza kwa maoni yako ikiwa ilikuwa busara kwa Ashua kumkataa Majoka kimapenzi kama njia ya kumthibiti Sudi. (alama 5)

c) Kwa kutolea mifano, onyesha sifa na tabia za Tunu zinazofaa kuigwa na viongozi wa kike. (alama 10)

RIWAYA CHOZI LA HERI

Jadili maudhui ya nafasi ya mwanamke katika riwaya ya Chozi la Heri. (alama 20)

HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

*"Nasema nizikeni hapa."*

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Taja na uelezee sifa za mnenaji wa dondoo hili. (alama 6)

c) Fafanua maudhui yoyofe matano yanayoshughulikiwa katika hadithi hii, (alama 10)

FASIHI SIMULIZI



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

7. (a) Lakabu ni nini ? (alama 2)

(b) Eleza sifa nne za lakabu (alama 8)

(c) Eleza umuhimu wa lakabu (alama 10)

## MTIHANI WA 18

TAMTHILIA KIGOGO

a. Fafanua mazingira ya Sagamoyo (alama 10)

b. Ni mambo yapi yanayofanya Sagamoyo kutokuwa na maendeleo? (alama 10)

au

"Utetezi wa haki za Wanasagamoyo umefanikishwa na Wahusika kadhaa katika tamthilia ya Kigogo. " Thibitisha. (alama 20)

RIWAYA CHOZI LA HERI

*"Hakuna msiba usiokuwa na mwenzake."*

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

b) Eleza tamathali ya usemi katika dondoo hili.

c) Eleza sifa za anayerejelewa.

d) Fafanua matatizo wanayoyapitia wakimbizi wa ndani kwa ndani.

HADITHI FUPI

Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine

a) Mashaka ni jina la kimajazi katika hadithi ya "Ndoto ya Mashaka". Jadili. (alama 10)

b) Onyesha namna asasi ya ndoa ilivyoshughulikiwa katika hadithi hii. (alama 10)

*"Kumekucha na makuchakucha yake."*

a) Fafanua ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya "Ndoto ya Mashaka" (alama 14)

b) Eleza umuhimu wa mhusika Mashaka. (alama 6)

FASIHI SIMULIZI

a) Maigizo ni nini (alama 2)

b) Andika sifa za maigizo (alama 4)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851706)

c) Ngomezi ni nini (alama 2)

d) Taja aina mbili za ujumbe ambazo zinaweza kuwasilishwa na ngomezi (alama 2)

e) Andika sifa za ngomezi (alama 4)

f) Miviga ni nini (alama 2)

g) Miviga ina umuhimu gani? (alama 4)

USHAIRI

*Jibu swali la 1 au la 2*

Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali

1. Tunda la elimu zote, wanasema wanazuoni Ni kwamba mtu apate, kumtambua manani Ndipo hadhi apate, akumbukwe duniani.

2. Elimu bila ukweli, haizidi asilani
Giza na nuru muhali, katu havitangamani
Uwongo ufe kweli, itue nuru moyoni

3. Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani
Ni bora yashinda mali, taji la wanazuoni
Elimu njoma miali,langazayo gizani.

4. Mtu hachomwi na mwiba, na viatu miguuni Ulimwengu una miiba, tele tele majiani Elimu ukiishiba, u salama duniani.

5. Wafu ni wasiosoma, watazikwa ardhini
Hai ndio maulana,wapaao maangani
Elimu jambo adhima, aso nayo maskini.

6. Toa wakfu ujana, elimu ukitamani
Na uwe mzee sana, kujua usijihini
Elimu ni jambo adhima, aso nayo maskini

7. Elimu ina malipo, utoyalipwa mwishoni



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Pale uitafutapo, ujira usitamani
Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.

8. Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni
Wao wameongolewa, na ni taa duniani
Kweli wanapoijua, watoe bila kuhuni.

9. Elimu bila amali, mti usio majani
Haumtii kivuli, aukaliaye chini
Inakuwa mashkeli, wa kughuri insane.

**Maswali**

a) Toa kichwa mwafaka kwa shairi hili (alama 2)
b) Taja aina na bahari ya shairi (alama 3)
c) Eleza umbo la shairi (alama 6)
d) Fafanua maudhui katika ubeti wa tatu na wa saba (alama 6)
e) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya tutumbi/nathari. (alama 3)

SWALI 2

1. Punda kalibebe gari gari limebeba punda
Mwalimu ana pakari muashi vyuma adunda
Jaji gonga msumari sonara osha vidonda
Kinyume mbele

2. Saramala ahubiri muhunzi tiba apenda
Mganga anaabiri bahari anakwenda
Hata fundi wa magari anatomea vibanda
Kinyume mbele

3. Wakili anahiyari biashara kuitenda
Mtazame asikari akazakaza vitanda
Mkulima mashuhuri jembe limeshamshinda
Kinyume mbele

4. Apakasa daktari ukili anaupinda
Saveya kawa Jabari mawe anafundafunda
Hazini wa utajiri mali yote aiponda
Kinyume mbele

5. Msemi huwa hasemi wa inda hafanyi inda
Fahali hawasimami wanene waliishakonda
Walijitia utemi maisha yamewavunda


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Kinyume mbele

6. Kiwapi cha kukadiri    twavuna shinda kwa shinda
Tele haitakadari    huvia tulivyopanda
Mipango imehajiri    la kunyooka hupinda Kinyume
mbele

<u>MASWALI</u>

a) Andika anwani mwafaka ya shairi hili (alama 1)
b) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)
c) Taja vinyume kumi vinavyorejelewa katika shairi (alama 5)
d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari (alama 4)
e) Onyesha jinsi mwandishi ametumia idhini ya ushauri (alama 4)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (alama 2)
   (i) Pakari
   (ii) Apakasa

## MTIHANI WA 19

USHAIRI

<u>SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI.</u>

1. Naja sasa ni ndiyani ,naja kwetu mzalendo
Naja nirudi nyumbani ,nilowekwa nako kando
kwetu' mi nakutamani ,kulo na mwingi uhondo
Nijaye ni ile nyundo ,misumari hadharani

1. Naja kwingine juwapi ,kulojaa langu pendo ?
Henda nende kwinginepi,sawa nako kwa muundo?
Kaa kwingine anapi ,ela kwenye lakwe gando?
Nijaye ni ile nyundo ,msumari hadharini.

2. Naja nije rudi papo ,panigendeme mgando
Ningaambiwa kwetu hapo ,kwamba kwanuka uvundo
Sitakwenda penginepo ,'tarudi kuko kwa mwando



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Nijaye ni ile nyundo,misumari hadharani .

3. Naja sitapakimbiya ,ningambwa kuna vimondo
   Takujakuvilekeya , vinganijiya kwa rundo
   Nilipozawa ‘tafiya,sikimbii kwenda kando
Nijaye ni ile nyundo,misumari hadharini.

5 Naja hiwa ‘mekomaa ,kuzidi nilivyo mwando
   Tena nnajiandaa,kwa fikira na vitendo
   Kwetu nije kuifaa, na kitilioya pondo
   Nijaye ni ile nyundo ,misumari hadharini.

6 Naja na ingawa maja ,siwaekei mifundo
   Moyo wangu ushatuja ,mawi nalotendwa mwando
   Ela wataoningoja ,na vyao viwi vitendo
   Nijaye ni ile nyundo,misumari hadharini.

(a) Eleza jinsi ‘ uzalendo’ wa mshairi unavyo jitokeza katika beti za 1 na 2 (alama 4)

(b) Fafanua jazanda zinazopatikana katika mshororo:

Kaa kwingine anapi,ela kwenye lakwe gando? (alama 2)

(c) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari. (alama 4)

(d) (i) katika ubeti wa 5 mshairi amebadilika.Eleza (alama 2

(ii) Ananuia kufanya nini pindi arudipo? (alama 2)

(e) Eleza ujumbe unaopatikana katika ubeti wa 6. (alama 2)

(f) Andika maneno haya katika Kiswahili sanifu; (alama 2)

(i) mwando

(ii) ningambwa

(g) Kibwagizo cha shairi kinampa sifa gani mshairi? (alama 2)

## HADITHI FUPI

## Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine

(a) *“Sekta ya elimu imekumbwa na changamoto katika jamii”.* Fafanua kauli hii ukirejelea diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine. (alama 20)

(b) *'Jazanda inatumika katika hadithi ya "Kidege ".'* Fafanua. (alama 20)

TAMTHILIA KIGOGO

*"Mtu hujichorea ramani yake ya maisha mwenyewe. Yatafakari hayo."*

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Taja na ueleze tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)

c) Ukirejelea tamthilia ya Kigogo, eleza ukweli wa dondoo hili (alama 1e).

RIWAYA CHOZI LA HERI

*"Mabadiliko ni aushi*". Huku ukirejelea riwaya ya Chozi la Heri, thibitisha kauli hii. (alama 20)

FASIHI SIMULIZI

7. a) Ngomezi ni nini? (alama 2)

b) Eleza sifa tano za ngomezi ? (alama10)

c) Fafanua kasoro nne zinazohusishwa na ngomezi, kama kipera cha fasihi simulizi? (alama 8)

MTIHANI WA 20

USHAIRI

<u>*Soma shairi hili kasha ujibu maswali*</u>

'Mepewa macho nione nami sitayatumbuwa
Vikondefu na vinene nipate kuvichunguwa
Pema na penye swenene la kuwa na kutokuwa
Vipe nione mavune nambie raha muruwa?
Nimepewa macho sitayatofowa!

'Mepewa na sikiyo katu sitolikwanyuwa
Ya kweli na singiziyo nipate kuyabaguwa
Vipi 'sikie kemeyo nite sauti ya hawa?
Binadamu yake nia tamu pate 'sikia



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851796)

‘Mepewa sikiyo        sitalibanduwa!

‘mepewa na pua hino        kamwe sitaing’watuwa
Vioza pia vinono        puani kunukuliwa
Mnaso wake na vuno        na mnuko kuchenguwa
Vipi nisinuse pano        na kule kuna shuruwa?
Mepewa na puwa        sitaimeguwa!

‘Mepewa huu ulimi        nami sitaunyotowa
Nitakalamu usemi        wenye nia na afuwa
Na maonjo vya vinyemi        sina budi kuchaguwa
Vipi nisionje kumi        na naoja nimecheuwa?
‘mepewa ulimi        sitausokowa!

Nimepewa na hii ngozi        Katu sitaibanduwa
Hisia zinajalizi        zipate kusisimuwa
Nyengine za maliwazi        nyengine za kubabuwa
Vipi nisihisi twezi        ngozi ikibabuliwa?
‘Mepewa na ngozi        sitoichunuwa!

Nimepewa na nadhari        kupima na kupimuwa
Nende mwendo wa kadiri        wa kuhisi na kujuwa
Wa ku’zepuka hatari        zote zinokusudiwa
Vipi mimi nihiyari        hisia zangu kutwawa?
‘Mepewa nadhari        sitoiondowa!

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (alama 1)

(b) Shairi hili ni la bahari gani? (alama2)

(c) Eleza mtindo wa shairi hili (alama4)

(d) Eleza ni kwa nini mshairi ametumia ritifaa katika shairi hili (alama2)

(e) Eleza muundo wa shairi (alama 4)

(f) Huku ukitoa mifano eleza vile mshairi alivyotumia uhuru wa kishairi (alama2)

(g) Taja 'hisi'nne zilizotajwa na mshairi. (alama 2)

(h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi. (alama 3)

(i) Swenene

(ii) vioza

(iii)Twezi

TAMTHILIA KIGOGO

a) Onyesha jinsi hali ya taharuki imetumika katika tamthilia ya Kigogo.

b) Mtindo wa uwili umetumika katika tamthilia hii.' Thibitisha kauli hii.

RIWAYA CHOZI LA HERI

*"Si kufua, si kupiga deki, si kupika, almradi kila siku ilikuwa na adha zake."*

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

a) Eleza mbinu ya lugha ambayo imetumika kwenye dondoo. (alama 2)

b) Eleza kwa kifupi madhila aliyoyataja msemaji. (alama 2)

c) Eleza kwa mifano jinsi haki za watoto zimekiukwa katika riwaya ya Chozi la Heri.

(alama 10)

HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

*a) 'Maudhui ya mapenzi yameshughulikiwa vilivyo katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.'* Thibitisha kauli hii. (alama 20)

*b) "Umdhaniye ndiye kumbe siye."* Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi zozote tano katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine. (alama 20)

haulambwi. (alama 12)

FASIHI SIMULIZI

(a) Lakabu ni nini ? (alama 2)

(b) Eleza sifa nne za lakabu (alama 8)

(c) Eleza umuhimu wa lakabu (alama 10)

## MTIHANI WA 21

USHAIRI

SWALI LA LAZIMA

*Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo*

Walimwengu nambieni,
Mie nipate fahamu
Hawamo vijana wetu
Meingilia yapi mambo,
Hulkazo hawa wana, tewengu zatia waj,
Sampuli ya hivi vikembe,
Lipi jama nelimisha

Watembea kwa vihindo
Mirindimo ardhi tia,
Ole wako kikutana, nao hawa masultani,
Takupita ja risasi, vikumbo nusura upigwe,
Wanadi maisha ni shoti
Wapapie kwa haraka

Viatu vya chuchumia, ati mbingu wafikila,
Magotini vyabisha hodi, waungwana waole,
Vishati vya kuninginia,
Matumboni ja kima,
Waso haya wana haa,



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Wana mji wao ati,

Kikutana nao njinai,
Manywele taambani, maashiki wa rasta,
Bbmal waabudu, ndio jagina wao wana,
Ziki lao la kisasa, lashangaza weni waja,
Sautiyo maskio,
Kusikiza ole wako, tajipata umepokewa,

Na hapa jahazi, langu ufukoni lafikile,
Enyi vijana pilika,
Ya kisasa kufuata,
Bila hadhari si haki,
Tuchuje yenye tijara,
Ya izara tupuzile,
Heshima tudumishe, tamaduni tuienzi.

Maswali

(a) Kwa kutoa mifano, eleza mambo mshairi analalamikia (al.3)

(b)Eleza ukitoa mifano namna utungo huu umezingatia kaida za ushairi kimuundo (al.3)

(c) Andika mfano moja wa (al.4)

(i) Mstari mishata

(ii) Mstari kifu

(d) Eleza namna uhuru wa ushairi unavyodhihirika katika utungo huu

(e) Andika ubeti wan ne kwa lugha tutumbi (al.4)

(e)Andika toni ya shairi hii (al.2)

(i) Libasi



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI [illegible])

(ii) Tijara

HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE: "Shogake Dada ana Ndevu" (Alifa Chokocho)

*"Halindwi, hujilinda yeye mwenyewe. Hujilinda ndani sikwambii nje."*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Onesha tamathali mbili za usemi kwenye dondoo. (alama 2)

(ch) Fafanua sifa saba za anayerejelewa katika kauli hii. (alama 14)

*Kwa kurejelea hadithi zozote tatu katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine, jadili vile waandishi walivyoshughulikia suala la mapuuza katika jamii.* (alama 20)

TAMTHILIA: KIGOGO

*"Si dawa ya deni ni kulipa?"*

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Onesha umuhimu wa msemaji katika kuijenga tamthilia ya Kigogo. (alama 4)

(ch) Jadili malipo mbalimbali ambayo wahusika tofauti walilipwa kwa uovu waliowafanyia wenzao katika eneo la Sagamoyo. (alama 12)

*Jadili mbinu ambazo Majoka anatumia kujidumisha mamlakani.* (alama 20)

RIWAYA: CHOZI LA HERI

"Hakujali kuwa amemwacha mwenzake akitapatapa na maumivu ya kusalitiwa." Onesha vile mwandishi ameshughulikia maudhui ya usaliti. (alama 20)

FASIHI SIMULIZI

(a) Eleza maana ya ngomezi (alama.2)

(b) Eleza sifa za ngomezi (alama.4)

(c) Toa mifano ya ngomezi katika maisha ya kisasa (alama.4)

(d) Maghani ni nini? (alama.4)

(e) Fafanua maana ya vipera hivi vya fasihi simulizi

(i)vivugo (alama.2)

(ii) tondozi (alama.2)

(iii) Pembezi (alama.2)

(iv) Rara (alama.2)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

## MTIHANI WA 22

### SEHEMU YA A:  USHAIRI

1. Mbiu  naipulizia, kwa wa hapa  na wa ng’ambo,
Kwani ngoja ‘mesikia, inaumiza matumbo,
Kwa  upole  sitafyoa, hata kama kwa kimo mbo,
Yafaa jihadharia, maisha yas,ende kambo;

2. Maisha yas’ende kombo, kututoa yetu ari,
Zingatia haya mambo, wetu walezi mukiri,
Kuwa wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri
Watunzeni na maumbo, msijezusha hatari

3. Msijezusha hatari, na nyingi hizi zahana,
Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama
Twaeleza kwa uzuri, matendoyo  yatuuma.
Watoto tunayo mori, mi lini mtajakoma?

4. Ni nani mtajakoma, na pombe ziso halali?
Sio baba sio mama, mbona ny’hamtujali
Mwafa ja nzi twasema, mwatuacha bila hali
Hangaiko  acha nyuma, kwani hamuoni hili?

5. Kwani hamuoni hili, kila mwapigana
Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona
Mwatusumbua akili, twaumia tena sana
Achene na ukatili, kwani upendo hamna,

6. Kwani upendo hamna, Kama mbwa mwatuchapa
Mwatuchoma sisi wana, mioyetu yatupapa
Pa kujificha hatuna, tumebaki  tukitapa
Maisha hamu hayana, timevunjwa na mifupa.

7. Tumevunjwa na mifupa, hata leo uke wetu,
Mwatubaka na kuapa, kutung’ata nyi’ majitu,
Maisha hatujakopa, fahamu  mkosa utu,
Hayo makeke na pupa, mtakoma utukutu,

8. Mtakoma utukutu, na kutumia mikiki, Na tabia zenye kutu, tumechoka nay chuki, Hatutakubali katu, kutendewa yenya siki, Serikali fanya kitu,



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724251796)

kwani nasi tuna haki.

**Maswali**

a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama 2)
b) Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)
c) Taja nafsi neni katika shairi hili. (alama 1)
d) Eleza bahari nne zinazowakilishwa katika shairi hili. (alama 4)
e) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
f) Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)
g) Huku ukitoa mfano taja mfano mmoja wa uhuru wa mshairi ambao umetumiwa katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU YA B:

RIWAYA: CHOZI LA HERI (ASSUMPTA K MATEI)

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. Jamii ya Chozi la Heri ni taswira ya jinsi ukabila unavyoathiri bara la Afrika.Jadili (alama20)
3. Malezi ya watoto katika riwaya ya Chozi la Heri ndicho kitovu cha ufanisi na matatizo yote yanayowapiku watoto (alama 20)

## SEHEMU YA C: TAMTHILIA KIGOGO PAULINE KEA

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Oooh bebi, miaka yaenda mbio sana, nayo sura yako inachujuka……"
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Mhusika anayehusishwa na wimbo huu ana msimano gani wa kimapinduzi? (alama 8)
   c) Taja sifa zozote nane za muhusika huyu (alama 8)
5. Tamthilia ya 'Kigogo' ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika. Thibitisha. (alama 20)

## SEHEMU YA D: HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINEZO

**Jibu swali la 6 au la 7** 6.

**"Rasta twambie bwana!"**

a) Weka dondo katika muktadha (ala 4)
b) Taja mbinu zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili (ala 2)
c) Ni kwa vipi mzungumziwa anamchukulia mwalimu mkuu kama hambe? (alama 4)
d) Je, mtihani wa maisha ni amwani faafu ya hadithi hii. (alama10)

7. Jadili mashaka ya Mashaka katika hadithi ya "Ndoto ya Mashaka" (alama 20)

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMJULIZI

8.

a) Fafanua mambo yanayochangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (alama 10)
b) Eleza maana ya lakabu. (alama 2)
c) Sifa za lakabu ni zipi? (alama 4)


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

d) Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii. (alama 4)

## MTIHANI WA 23

SEHEMU YA A – RIWAYA: *CHOZI LA HERI* SWALI LA LAZIMA

1. Jadili sifa za wahusika wafuato na umuhimu wao
   a) Ridhaa (alama 10)
   b) Mwangeka(alama 10)

SEHEMU YA B – TAMTHILIA: *KIGOGO*

**Jibu swali la 2 au 3**

2.“Dalili ya mvua ni mawingu, lazima tuwe macho”.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)

(c) Ushauri uliotolewa na msemaji baadaye kama njia mojawapo ya kuwa macho ni wa kidhalimu. Fafanua. (alama 4)

(d) Eleza namna unafiki wa msemaji na upumbavu wa mnenewa unavyodhihirika katika muktadha wa dondoo hili.(alama

(e) Onesha jinsi ukweli wa kauli hii ulivyojitokeza baadaye katika tamthilia. (alama 4)

3. Jadili migogoro inayojitokeza katika tamthilia ya *kigogo*, kisha utathmini namna ilivyosuluhishwa. alama 20)

SEHEMU YA C:HADITHI FUPI: *TUMBO LISILOSHIBA*

**Jibu swali la 4 au 5** 4. “Kesho kama sote tutaamka salama……….kama tutafungua milango ya nyumba zetu”….

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4) (c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)

(d) Hadithi hii inaakisi mambo mengi yanayotendeka katika bara la Afrika. Taja mambo sita (alama 6)

5. Ukengeushi huzorotesha maendeleo ya kijamii. Jadili kauli hii ukirejelea hadithi ya ‘Mkubwa’. (alama 20)

SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI

6. (a) Eleza vipengele vitano vya fasihi simulizi ambavyo hujitokeza katika fasihi andishi.(alama 10)

(b ) Fafanua sifa tano za ushairi simulizi. (alama 10)

SEHEMU E: USHAIRI

**7. Soma mashairi haya kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Shairi A

Umekata mti mtima
Umeangukia nyumba yako
Umeziba mto hasira
Nyumba yako sasa
mafurikoni Na utahama



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Watoto kuwakimbia.

Mbuzi kumkaribia chui
Alijigeuza panya
Akalia kuliwa na paka kichwani
Mchawi kutaka sana
kutisha Alijigeuza samba
Akalia na risasi kichwani.

Jongoo kutaka sana kukimbia
Aliomba miguu elfu
Akaachwa na nyoka

Hadija wapi sasa utakwenda
Bwanako kumpa sumu? Hadija
umemshika nyoka kwa mkia,
Hadija umepita nyama ya Punda.

Shairi B
Piteni jamani, Piteni haraka
Nendeni, nendeni huko mwendako
Mimi haraka, haraka sina,
Mzigo wangu, mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuweka.

Vijana kwa nini hampiti?
Kwa nini mwanicheka kisogo?
Mzigo nilioubeba haupo kichwani
Lakini umenipinda mgongo na
miguu Na lazima nijiegemeze,
kichwani Chini nendeko.

Haya Piteni! Piteni! Haraka! Heei!
Mwafikiri mwaniacha nyuma!
Njia ya maisha ni moja tu
Huko mwendako ndiko nilikotoka
Na nilipofikia wengine wenu
Hawatafika.

Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati
Lakini kama mnepita mbele
Na uso wangu kuutazama Ningewambia siri ya miaka mingi.

<u>MASWALI</u>


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724851796)

(e) Haya ni mashairi ya aina gani? (al.1)
(f) Washairi hawa wawili wanalalamika. **Yafafanue** malalamishi yao. (al.4)
(g) Onesha vile kinaya kinavyojitokeza katika tungo hizi mbili. (al.6)
(h) Kwa kurejelea shairi 'B'**eleza** maana ya: (al.3)
(a) mzigo
(b)Siri
(c) Niko nyuma ya wakati
(e) **Andika** ubeti wa kwanza wa shairi 'A' kwa lugha nathari (alama 4)
(f) Uhuru wa mshairi umetumiwa vipi katika shairi 'B' (alama 2)

## MTIHANI WA 24

### SEHEMU A: USHAIRI

Jinalo limetukuka, kutoka jadi mwanzoni
Milele hutadunika, hata kwa pigo vitani
Ulugha uloumbika, muundo wa wasitani
Hakuna wa kukuponda; mwana mwema Kiswahili

Kila anokuutamka, hukunyambua kifani
Hasemi kuhakahaka, ja mwana wa uchangani
Vitabuni kitumika, hupumbaza nyoyo ndani
Na milele hutavunda, mwana mwema Kiswahili

Mja akikitamka, mwenyeji ama mgeni
Msikizi huridhika, ungiavyo mdomoni
Humwondokea wahaka, ukapenya sikioni
Hapana wa kukushinda, mwana mwema Kiswahili

Vitabuni huchipuka, ukashawishi maoni
Hutuwili kila rika, wakatukuza nishani
Nami ninakuzindika, usambae duniani
Hawapi wa kukukinda, mwana mwema Kiswahili

Kiswahili tokatoka, uenee duniani Kila
baidi we fika, pembe'ne ulimwenguni
Ukizamishwa ibuka, uabiri kila kani
Hazuki wa kukushinda, mwana mwema Kiswahili

Kwa vina umeumbika, umeshinda kilatini
Na mizani za mwafaka, utamkwapo wimboni
Nishani nitakutwika, utamalaki maoni
Hazuki wa kukushinda, mwana mwema Kiswahili

Nakuaga mtukuka, Kiswahili mwenye mboni


© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

Kitabuni nakuweka, wasome mamilioni
Utuwe kusalimka, maombi ya mwarandani
Hayuko wa kukufyanda, mwana mwema Kiswahili

*Maswali*

1 Pendkeza anwani inayofaa shairi hili (al. 2)
2 Ni mbinu gani ya lugha ambayo Imetumika katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa pili (al. 2)
3 Eleza toni ya shairi hili (al. 2)
4 Uhuru wa kishairi umetumikaje katika shairi hili (al. 3)
5 shairi hili linaweza kuwekwa katika bahari gani. Taja mbili (al. 2)
6 Eleza muundo wa shairi (al. 4)
7 Mshairi anatoa ujumbe gani katika ubeti wa sita (al. 3)
8 Eleza maana ya: (al. 2)

- Na milele hutavunda
- Kiswahili mwenye mboni

SEHEMU B :CHOZI LA HERI

2."Haiwezekani! Hili haliwezekani! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Taja mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili (alama 2)
c) Eleza athari za usemi unaopatikana katika dondoo hili (alama 14) AU

3 .Eleza jinsi mbinu ya jazanda ulivyotumika riwayani (al.20)

SEHEMU C:KIGOGO

4 " Mguu huu ni wako"

- Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
- Ni tamathali gani ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. Eleza maana yake (al.2)
- Msemewa alipewa ahadi zipi (al. 5)
- Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji (al. 9)

5 Eleza mbinu ya

- Majazi (al.10)
- Kinaya (al.10)

SEHEMU D:TUMBO LISILOSHIBA

6. Kwa kuzingatia hadithi zozote tano eleza uozo wa jamii kama unavyojitokeza katika tumbo lisiloshiba (Diwani)

7 "Kesho panapo majaaliwa. Kesho kama sote tutaamka…….. kama tutafungua milango ya nyumba zetu zinazosimamia juu ya ardhi hii adhimu…"

a Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4) b
Eleza sifa nne za msemaji (al. 4) c)
Taja mbinu zozote mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili (al. 2) d
Kwa kurejelea hadithi nzima onyesha namna jamii ya kisasa ina tumbo lisiloshiba (al. 10)

SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI

8 a Eleza maana ya miviga (al. 2)
B Taja mifano mitano ya miviga katika jamii za kiafrika, kabla ya kuja kura wamishenari (al 5)
C Eleza majukumu ya miviga (al. 5)



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

D Taja na ueleze vitambulishi vya fasihi simulizi (ala8)

## MTIHANI WA 25

CHOZI LA HERI

1. " Kwa kweli ni hali ngumu hii"
   a) Weka dondoo katika muktadha wake. (alama4)
   b) Ni hali gani ya msemewa inayorejelewa kwenye dondoo. (alama16)

TAMTHILIA (KIGOGO)

Jibuswali la 2 au 3

2. "Wao na mimi ni ganda la muwa la juzi"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

b) Tambua mbinu ya uandishi iliyotumika katika dondoo hili (alama2)

c) Thibitisha kuwa wahusika kadhaa wanalinganishwa na ganda la muwa katika tamthilia (alama14)

*AU*

3. Anwani "KIGOGO"imetumika kitashtiti kumkejeli Majoka. Thibitisha (alama20)

HADITHI FUPI – TumboLisiloshibanaHadithiNyingine

Jibuswali la 4 au 5

4. Jadili jazanda za anwani katika hadithi zifuatazo
   a) Shibe Inatumaliza (alama8)
   b) Mtihani wamaisha (alama6)
   c) Mkubwa (alama 6)

*AU*

5. *MAPENZI YA KIFAURONGO*

   "Kutazama shule za vijiji ni kumwibua bingwa katika mtihani wa kitaifa ni kama kutarajia kupata maziwa kutoka kwa kuku."
   a) Eleza muktadhawa dondoo hili (alama 4)
   b) Tambua mbinu moja ya lugha kwenye dondoo hili. (alama 2)
   c) Jadili maudhui yafuatayo katika hadithi hii
      i) Mabadiliko (alama 5) ii) Uozo (alama 5) iii) Shaka (alama 4)

FASIHI SIMULIZI



© 2019 BWANA CHEPKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

6. a) Fafanua mchakato wa uwasilishaji wa vitendawili. (alama4)

c) Linganisha na ulinganue vitendawili na methali. (alama10

d) Toa sababu sita za kudidimia kwa fasihi simulizi. (alama6)

***SEHEMU YA E: USHAIRI***

*7. Soma shairilifuatalokishaujibumaswali.*

Moyohaukongi:
Haidhuruuwewamwanadamu
Au wanyamamwitu.

Japomajiyamyumbishe
Kandonimwababahari
Kizeeutamwona
Kwanguvuzauchawiwamoyo
Mawimbiniakisukwasukwa
Mithiliyajahazilililochoka
Kwaurefuwa safari:
Ingawaatabamizwamatumbwawen
i Na yakeserunimajikuitwaa
Atang’ang’anakuidakajapokwashida
Na majinikuelea Kama
anayeyatishakuwa
Badosihayamisuliipo.

Basiajabuusione
Pakamaziwakunywa
Katikauzima wake
Au bi kizeekichwaakiyumbisha
Kwamliowaala
Amanyamakupaniakula
Japojino la mwisho
Liling’okajuzi.

Moyohaukongikwamsukumowawakati:
Ni misuliinokonga.
Moyo, simbawawakati.

a) Hili ni shairi la aina gani? (Alama 2)

b) Eleza muundo wa shairi hili. (Alama 4)

c) Kwa nini mshairi anaeleza kuwa moyo haukongi? (Alama 4)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

d) Tambua mishororo baki kwenye shairi hili. (Alama 2)

e) Eleza mbinu mbili za idhini ya mshairi kwa kurejelea shairi hili. (Alama 2)

f) Eleza toni ya shairi hili. (Alama 2)

g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (Alama 4)



© 2019 BWANA CHERKWONY (KWA NA JIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706)

# For more:

👉🏿*Friendly high school & primary Notes*

👉🏿 *Primary-secondary school exams*

👉🏿*2020 updated schemes of work (primary-secondary)*

👉🏿*All KASNEB notes(CPA,CICTCIFA,CS,ATD,ICT &IT)*

WhatsApp/Call/sms Mdm.Mariam @ 0746711892